Ninawezaje Kushinda?

Hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa maombi.

Baba yetu, tunakushukuru, asubuhi ya leo, kwa wakati huu mzuri wa kukutana tena, na kufunguliwa kwa Neno la Bwana, kuliweka hapa mbele zetu. Na—na kwa maombi sasa, ili kwamba Roho Mtakatifu atachukua kile alicho Mungu, na kutupa sisi, kusudi tuondoke mahali hapa pa kuabudia leo tukiwa na mioyo michangamfu iliyojaa furaha. Kuona nguvu Zako kuu za ukombozi, Bwana, jinsi zinavyowakomboa wafungwa na kuwaweka huru, zinatujulisha "mambo yaliyokuwako, na yaliyopo, na yatakayokuja." Nasi tunakushukuru tu kwa ajili ya mambo haya.

2 Tunaomba ya kwamba utatubariki tunapojifunza Neno Lako sasa pamoja. Na tutakapoondoka, na isemwe mioyoni mwetu, tunaposafiri njiani, "Mioyo yetu iliwaka ndani yetu wakati Yeye, Roho Mtakatifu, alipozungumza nasi tulipokuwa njiani."

3 Bariki kila mhudumu leo, kila mahali, watumishi Wako wanaoitetea Hii, Kweli Yako. Yajibu maombi yao kwa ajili ya wagonjwa. Iponye miili migonjwa ya wale wanaoteseka.

4 Bwana, tungeomba ya kwamba ungetoka uende miongoni mwa watu na kuutafuta ule uzao uliochaguliwa tangu zamani huko nje, Bwana, na kuuleta huku, kwa njia fulani, kusudi Nuru ianguke njiani, Bwana. Kwa kuwa, tunaamini ya kwamba saa inaenda sana, jua linatua upesi magharibi, ndipo karibuni itakuwa kwamba "hakutakuwa na wakati baada ya haya." Wakati na Umilele vitaungana pamoja wakati Mungu na watu Wake watakapoungana pamoja. Na tunaomba, Mungu, ya kwamba, kwenye wakati huo, ya kwamba tutahesabiwa miongoni mwa wale watakaounganishwa katika Kristo, wanaoitwa Bibi-Arusi Wake.

Tusaidie, leo, tunapojitayarisha, huku hatujui kesho ina kitu gani, bali tuko tayari kupokea chochote, Bwana, kadiri tujuavyo sisi, kile ulicho nacho kwa ajili yetu. Tuko tayari kukipokea. Tunaomba baraka hii kwa ajili ya utukufu wa Mungu, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Mwaweza kuketi.

5 Hakika nilikuwa na furaha, asubuhi ya leo, wakati nilipoingia na kuona ya kwamba wa—watu walikusanyika kwa ajili ya ibada ya Bwana. Nasi tunatoa sasa tangazo kwa ajili ya usiku wa leo. Kutakuwako na ibada ya uponyaji usiku wa leo. Tutakuwa tunawaombea wagonjwa, usiku wa leo. Muda kidogo tu uliopita, wao . . .

6 Nilipoingia, Billy, mwanangu, aliniambia, alisema, "Yupo mu—muungwana hapa, ambaye ni maskini tu ambaye ameendesha gari kutoka mbali." Kisha akasema, "Ni—nilimweka chumbani, Baba."

7 Ni—nilifika nimechelewa jana usiku, na—na sikuweza kusoma sana kwa ajili ya somo la shule ya Jumapili ambalo nilikuwa nizungumzie, asubuhi ya leo. Kwa hiyo nilichukua baadhi ya mihtasari midogo ambayo nilichukua kutoka kwa yale niliyomsikia ndugu mmoja akisema, na nikatoa somo kutoka kwa hayo, kusudi kwa namna fulani nipate somo la shule ya Jumapili asubuhi ya leo; na wakati tukijitayarisha, na kujitayarisha kwa ajili ya ibada ya jioni.

8 Basi Billy akasema, "Kuna mtu kule ndani ambaye ni mgonjwa." Kasema, "La—la—laiti ungepitia kule na kumwona." Kwa hiyo, niliingia kwenye hicho chumba hivi punde. Na ndugu mmoja wa karibu rika langu, na mkewe, wameketi mle ndani. Ndipo Roho Mtakatifu akashuka miongoni mwetu chumbani mle hivi punde.

9 Wazieni tu, kugusia tu ibada ya uponyaji, naye Huyo hapo. Unaona? Naye akamwambia ndugu huyu yote aliyokuwa amefanya, na yale aliyokuwa akifanya, na ni kitu gani kilisababisha shida yake, na mahali alikotoka, na yote kumhusu yeye. Na kulikuwa na kivuli kikubwa mno cheusi kilichoning'inia mle chumbani. Ndipo kukaanza kuingia mwanga zaidi, zaidi, zaidi, na zaidi, kisha Roho Mtakatifu akashika hatamu.

10 Sasa, nafikiri mtu huyo yuko katika . . . mahali fulani hapa nyuma sasa. Yeye na mke wake labda hawawezi kuingia jengoni, bali walisema watakaa, kwa vyovyote vile, kwa ajili ya ibada. Wanatoka huku karibu, karibu na Yakima, Washington, nao wakaja kwa gari. Naye ni mhudumu wa Injili.

Lakini kuona tu neema ya—ya Mungu pale! Ambapo, mtu huyo alikuwa hospitalini naye alitibiwa na kila kitu. Roho Mtakatifu akifunua haya yote. Wakati, madaktari wakijaribu sana kufanya kila walichoweza, labda, kwa ajili ya mtu huyo, lakini ilichukua tu huo mguso fulani mdogo kutoka kwa Mungu, kubadilisha mambo. Matibabu ya mshtuo ni sawa, lakini kwa namna fulani ni kama kile tungeita "kudunga sindano gizani," mwajua. Wewe, huenda ikakufanya mgonjwa zaidi, unaona, maana ungesahau kila kitu ulichowahi kujua, wakati wakiweka dawa hiyo ndani yako. Lakini Bwana Mungu, jinsi ambavyo neema Yake na rehema! Na hata kabla sijatamka neno moja la maombi kwa ajili yake, tayari ulikuwa umekwisha. Unaona? Ilichukua tu kile kitu fulani cha Mungu, ule mguso fulani, kufanya hivyo.

Sipaswi kusema jambo hili. Naam. Ningeangalia, nimwone mtu huyo sasa. Vema, sikujua kama ungefaulu leo, ama hungefaulu.

11 Huko mashambani mahali ambako nimekuwa nikikaa, juma hili. Ni—ni—ninapenda marafiki wangu kule. Ni likizo ndogo kabla ya mikutano hii mikubwa, unaona. Nami naja nyumbani, kushuka kwenda kule chini na kutoka kwenda kuwinda kindi pamoja na ndugu hawa. Na familia hii, familia hizi, hasa, ninazokaa pamoja nazo kule chini, ni watu wazuri kweli. Na mtu huyo, ndugu halisi, marafiki, hao ni marafiki.

Na mmoja wao anapenda sana mbwa wa—wa kuwinda. Naye ana kizimba kilichojaa hao kule juu. Na—nami niliona mtoto wa mbwa mkubwa mzuri sana wa kuwindia kule chini, jamaa mdogo, alikuwa ni kile ninachoita hivyo, "nusu mbwa kwa urefu wa wima na mbwa wawili kwa urefu wa mlalo," unajua, aliyekuwa—aliyekuwa akikimbia-kimbia kule nyumbani. Nami nikawazia, "Jamani, hivi Joe si angetaka kuwa na kitu kama hicho!"

12 Na, hakika, huko Arizona, tusingeweza kumtumia. Angeingia kwenye mipungate, na huo ungekuwa ndio mwisho wake. Kwa hiyo basi nikasema, pia, "Huwezi kumchukua. Hawatumii mbwa kule ndani, sehemu hiyo ya nchi. Maana, wao, vema, kamwe wasingeweza kuwatumia. Wangeninii . . . pia, hali ya hewa, ha—hali hiyo ya nchi yenye mipungate, nao wangeuawa." Halafu basi, kweli, mbwa kule nje, m—mbwa mwitu, ama kitu fulani kingemwua, labda, hata hivyo, kama angetoka nje.

13 Kwa hiyo basi mtu huyu akaniambia, "Unaweza tu kumchukua." Lakini ni—nisingeweza kumchukua. Ni—nilithamini jambo hilo. Nikaja kutambua, alikuwa ni mmoja wa mbwa anaowapenda sana.

14 Na mtu huyu ana mke mzuri sana na watoto wadogo. Na hivi majuzi, alianza kurudi nyuma kwa gari lake, naye alikuwa na gari hili la Oldsmobile. Na maskini mbwa huyo ni mrefu tu *hivyo*, kitoto tu cha mbwa. Naye alimkanyaga moja kwa moja. Oldsmobile hiyo ikimkanyanga moja kwa moja mbwa huyo mdogo, mgongoni mwake *hapa*, ikamponda kabisa, ambapo mawe ya barabarani yalikuwa yamemchoma tumboni mwake hapa, unajua. Ndipo—ndipo maskini mke huyo, badala ya kumpeleka haraka mbwa huyo mdogo kwa huduma ya utabibu wa mifugo . . . Kweli, huduma ya utabibu wa mifugo ingemfanya alale mara moja, na kumwua. Unaona?

Palikuwapo na kijana mwanamume mwingine aliyekuwa pamoja nami. Na mara alipofika pale, alisema, "Huyo angelikuwa ni mbwa wangu, ningempiga risasi." Kasema, "Hivyo tu. Ati nimwache ateseke namna hiyo?"

15 Nikasema, "Vema, hebu na tusimpige risasi." Nikasema, "Hebu tungoje kidogo."

Nikamwondoa kila mtu, nami nikaenda nikamwombea. Maskini kitoto hicho cha mbwa kikanifuata sebuleni. Na yeye, [Kusanyiko linashangilia—Mh.] naam, yeye . . . Unaona? "Yoyote mnayotaka, mkiomba, aminini ya kwamba mnayapokea; yatakuwa yenu, mtapewa." "Yoyote." Huyo ni Bwana Mungu wetu. Sivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."] Yeye—Yeye ni wa ajabu sana na ni mzuri sana. Na hakika tunampenda, asubuhi ya leo; na tunamtarajia, na kujua.

16 Niliwaona, hivi majuzi, m—mtu na mke wazee, mama na baba wa mshiriki mzuri sana wa kusanyiko hi—hili la waaminio. Na mama huyo ni, loo, nadhani amekaribia umri wa miaka mia moja, na baba hivyo, pia. Na kwa karibu miaka kumi na miwili mtu huyu hajapata kusogea; kichalichali, amelala tu moja kwa moja. Ama, hawezi kulala kwa upande mmoja, wala chochote. Alilala pale kwa muda wa miaka kumi na miwili. Uzee tu! Na mama sasa ni karibu rika lake, nadhani, karibu na mia moja, na maskini mama huyo karibu amepoteza akili zake. Anafikiri mtu fulani anachukua yote aliyo nayo.

Nami niliangalia ninii . . . upande wa pili wa meza, kwa sisi wote, vijana kwa wazee, tulioketi pale. Nami nikasema, "Tunaelekea wapi? Tunafanya nini?" Na yule mama niliyekuwa nikikaa naye wakati huo, huyo alikuwa ni mama na baba yake. Nami nikasema, "Unaelekea upande huo, pia. Kweli kabisa, kila mmoja wetu." Unaona?

17 Wazia tu jambo hilo, kwa muda mfupi tu, kabla hatujaanza somo letu. Huko ndiko unakoelekea. Unashindania nini? Kusudi upate kuishi. Unaishi kwa kusudi gani? Kusudi upate kufa. Hivi si lingekuwa ni jambo la kijinga kama tusingelikubali sheria ya Mungu ya Uzima wa Milele? Tungeweza kuwazia nini? Ni—ni kitu gani kingekuwa niani mwetu, ambacho kingevutia usikivu wetu kutoka . . . kuelekea chochote? Vipi kama ulikuwa na dola milioni mia moja, na ulimiliki mkoa wa—wa Indiana, ama mkoa mwingine wowote, ama hata taifa, ama, kwa kusudi hilo, ulimwengu mzima?

Ukiishi muda mrefu kutosha, huna budi kufikia jambo hilo, pia. Unaona? Na daima, siku baada ya siku, kila wakati moyo wako unapopiga, unaelekea moja kwa moja kwenye jambo hilo. Unaona? Wewe, hakuna ushindi kwako. Uko upande wa kushindwa, na, wewe, huna budi kushindwa. Lakini kumbuka ile ahadi, ya kwamba, "Yeye atakayeyapoteza maisha yake kwa ajili Yangu atayapata." Sasa, ni kitu gani kingekuwa cha thamani zaidi kupata kuliko Uzima, ingawa ungalipata ulimwengu mzima kuwa ni mali yako? Lakini, kama uki—kama ukipata Uzima, umepata kitu kikuu kuliko vyote kinachoweza kupatikana. Ninataka kuninii . . .

18 Niliangalia upande wangu wa kushoto na nikaona tena, sasa hivi, kumbukumbu lingine la neema ya Bwana. Yapata majuma machache yaliyopita, niliitwa kwenye simu. Na mshiriki mzuri sana wa kanisa hili, ama wa mwili huu . . . Sitaki kuliita hili zaidi sana kama kanisa. Ni—ninataka kuliita hili, kwamba . . .

Kama vile nilivyokuwa nikizungumza na watu fulani, walisema, "Vema, wewe ni wa kanisa gani?"

Nikasema, "Mimi si mfuasi . . . "

"Wewe ni wa madhehebu gani?"

Nikasema, "Hakuna."

Kasema, "Vema, wewe ni wa kitu gani?"

Nikasema, "Ufalme."

19 Ufalme! "Na kwa Roho mmoja tunabatizwa kuwa katika Ufalme huo." Kwa Roho mmoja, sote, katika Ufalme huu! Yesu alisema, "Ombeni, 'Ufalme Wako uje. Mapenzi Yako yatimizwe hapa duniani, kama huko Mbinguni.'" Sasa, Yeye alisimama siku moja mbele ya Mlima wa Kugeuka Sura, akasema, "Amini nawaambia, ya kwamba wapo katika hawa wanaosimama hapa, ambao hawataonja mauti, hata watakapouona Ufalme ukija kwa nguvu." Ulionyeshwa mbele, kama tulivyolipitia hilo, Mlima wa Kugeuka sura. Nayo Biblia ilisema, "Ufalme wa Mungu umo ndani yenu." Kwa hiyo, hawa ni watu wa Ufalme wanaokiri ya kwamba haya si makazi yao. Haya si makazi yetu. Tunakutarajia Kuja kwa Mfalme, kuuanzisha ule Ufalme.

20 Niliitiwa jambo la dharura, ya ndugu m—mzee ambaye amekuwa ni kama baba kwangu. Na yeye . . . Sikuwa nimemjua kwa muda mrefu sana, bali ninakumbuka siku niliyomleta hapa kwa ajili ya ubatizo wa maji. Na mtu huyo hivi karibuni atakuwa na umri wa miaka tisini na moja. Na mke wake mzuri sana alinipigia simu, naye akiwa ni nesi, kasema, "Moyo wake ulikoma kabisa." Mbali na hayo, alikuwa na . . . Loo, ninauita . . . siwezi kukumbuka jina lake. Mshtuko wa moyo. [Dada fulani anasema, "Ugonjwa wa moyo."—Mh.] Ugonjwa wa mshtuko wa moyo. Asante. Ugonjwa wa mshtuko wa moyo, na kukoma kabisa kwa moyo. Daktari hakutoa matumaini yoyote, hata kidogo. Naye mtu huyo alikuwa anakufa, naye akaniita.

21 Ndipo niliingia kwenye maskini Ford yangu kuukuu, na nikaanza kwenda barabarani kuelekea Ohio, mbio nilivyoweza. Wala sikujua, gurudumu langu moja lilikuwa kombo, likapasua tairi ikatoka. Kwa hiyo basi mimi . . . nikifika kule. Nilipokuwa nikitoka kwenye kituo cha petroli, karibu saa tano. Nilikuwa nina wasiwasi juu yake. Ni—ninampenda. Nami ninajua, kama—kama ikiendelea, Bwana akikawia, mbona, punde si punde, itatulazimu kuachana.

22 Lakini, hilo halitavuruga Unyakuo, sasa. Unaona? La. Wanakuja kwanza, wakati huo. Hao wana majaliwa,

waliotutangulia. Watakuja kwanza. Unaona? Unaona? "Sisi tulio hai tutakaosalia, hata wakati wa Kuja kwake Bwana, hatutawatangulia ama kuwazuia hao waliokwisha kulala mauti. Parapanda ya Mungu italia; waliokufa katika Kristo watafufuka kwanza. Ndipo macho yetu yatakapowaona wapendwa wetu, ndipo tutabadilishwa, muda si muda, kufumba na kufumbua, nasi pamoja nao tutanyakuliwa pamoja." Unaona? Wale wanaoenda kwanza wana majaliwa kuliko wale walio hai.

23 Nilipokuwa nikitoka kwenye kituo hicho, kwenye saa tano tu, Roho Mtakatifu aliniambia, "Usiwe na wasiwasi juu yake. Utampa mkono, barabarani tena, naye atakuja kanisani," mtu mwenye umri wa miaka tisini na moja, akifa.

Nilipokutana na mke wake na wapendwa wake hospitalini huko Lima, waliniambia kuhusu hali yake. Nikaingia, nikamwangalia mle ndani. Akasema, "Lakini yeye ni kitu cha ajabu." Kasema, "A—alianza kupata nafuu, saa tano." Vema, na ningeninii . . . Bwana alikuwa amewaonyesha watu hao mambo mengi sana, wanajua ya kwamba sikusema tu jambo hilo. Kwa sababu, waliniambia kwanza, "Yeye alianza kupata nafuu." Walijua ya kwamba ningewaambia kweli.

24 Kwa hiyo, Jumapili iliyopita, nilipokuwa nikienda kwenye Mkahawa wa Blue Boar huko Louisville, ambako ninafikiri karibu asilimia themanini ya kusanyiko hili wanakusanyika Jumapili alasiri, kula, ni nani niliyemwona akishuka kuja barabarani? Nawaambia, moyo wangu ulitetemeka wakati nilipomwona Ndugu yetu Dauch akishuka kuja barabarani, jinsi hasa Yeye alivyoniambia. Nilimpa mkono, ba—barabarani.

25 Ndipo ni—nikarudi hapa kwa ajili ya Jumapili iliyopita usiku na kuzungumza juu ya somo la umoja, la *Kuungana Kwa Ishara ya Wakati*. Kwa hiyo . . . Ndipo basi hilo likatimiza jambo hilo, vile hasa Yeye alivyosema. Naye huyu hapa ameketi kanisani leo, papa hapa karibu na sisi, kama kumbukumbu la neema ya Mungu. Nilipokuwa nikimpa mkono chini ya hema, hema ya oksijeni aliyokuwa chini yake, nilisema, "Ndugu Dauch, utapona. Nitakuona kanisani tena. Hiyo, hiyo ni BWANA ASEMA HIVI." Unaona? Huyu hapa ameketi kanisani, papa hapa sasa, Ndugu Dauch.

26 Kama sijakosea, yule mhudumu niliyesema habari zake, muda mfupi uliopita, Roho Mtakatifu aliingia na kuyafunua mambo haya yote; akamwambia jinsi ilivyotukia, na akamwambia yale aliyofanya; jinsi ilivyotukia, jinsi lilivyotimia, yote ambayo yamekuwa yakitukia tangu wakati huo, hata kuhusu tabia ya familia yake, na yote kuhusu hayo. Na kumwambia, ya kwamba, "Imekwisha." Na huyo mhudumu ameketi papa hapa, kwenye mkono wa kulia. Ungeweza kuinua tu mkono wako, bwana? Pale, yeye na mke wake, hakika, sasa hivi.

Huyu hapa Ndugu Dauch ameketi, papa hapa sasa. Loo, jamani!

27 Hivi Yeye si ni wa ajabu? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] "Mambo hayo yaliyokuwako, yaliyopo, na yatakayokuja kutimia." Shahidi mmoja, wawili, watatu. "Mambo yaliyokuwako, yale umefanya; mambo yanayoendelea sasa; na mambo yatakayokuja kutimia." Na kila wakati, kikamilifu, kikamilifu juu ya Neno. Hilo ni Mungu tu anayeweza kufanya hilo. Loo! Hivi sisi hatuna furaha sana kwa ajili ya mambo haya? ["Amina."]

28 Sasa, sababu ya mimi kuchukua wakati mdogo tu wa ziada, ilimbidi Billy kwenda kumleta mke wake na mtoto wake mchanga. Naye alisema, "Baba, usianze kuhubiri mpaka nitakaporudi." Kwa hiyo, na—nafikiri amerudi sasa. Nami ninapaswa kuwa na kiasi kama hicho cha wakati, kwa vyovyote vile. Nami ninajaribu kuondokana na hizi saa nne za uchovu wa akili ambazo mimi huwaweka ninyi nyote hapa, na kuufanya dakika thelathini na tano, arobaini, unaona, na kujaribu kuudumisha.

29 Sasa, nilipongezwa wakati mmoja huko Chicago. Niliupunguza ukawa dakika thelathini, ama kitu kama hicho, dakika thelathini na tano. Na usiku wa Jumapili iliyopita ulikuwa ni wa dakika arobaini na tano tu. Billy alisema, "Kweli unafanya vizuri zaidi, baba. Kwa namna fulani ninakujivunia, kwa ajili ya jambo hilo."

30 Vema, labda, asubuhi ya leo, kuufanya kidogo uwe ni kama wa shule ya Jumapili, sitawaweka kwa muda mrefu kupita kiasi. Ndipo mnaweza kutoka na kwenda kula chakula chenu cha mchana, na kuomba, na kurudi usiku wa leo kwa ajili ya ibada za uponyaji. Tutafanya mstari wa maombi usiku wa leo na kuwaombea wagonjwa.

31 Sasa, kama mnawajua watu wowote hapa karibu, mahali popote, walio wagonjwa na wanataka kuombewa, waleteni hapa usiku wa leo. Mnaona? Kama itawabidi kuwaleta, kwa njia yoyote, waleteni hapa. Mnaona? Hilo ndilo jambo muhimu, ni, kuwaleta hapa usiku wa leo. Sote tunakutana pamoja. Kwa njia hiyo...Ni vigumu kuwaita, tukienda mahali baada ya mahali; ndipo unamwacha mtu fulani, nao wanakasirika. Bali kama ninaweza kuwaleta wote mahali pamoja, basi ningeweza kuwaombea. Sasa, kama mtaninii...Kama watu wanataka kuombewa, wao...Unasema, "Wataombewa?" Loo, hakika. Wataombewa. Waleteni humu. Bwana akipenda, tutakuwa hapa, tumwombee kila mtu. Maana, ninahisi ya kwamba huo mvuto wa tatu unaanza kutenda kazi, unaona, nda—ndani yangu. Na ni—ni—ninataka kumwombea kila mtu.

32 Sasa hebu tufungue, asubuhi ya leo Maandiko ya kale yanayojulikana ambapo kwa namna fulani niliyachagua

kwa haraka jana usiku, nikiwa nina usingizi mzito sana, na nikaandika Maandiko mengine machache ya kuambatana nayo. Na nikichukua kama kwamba ni nyongeza. Nilimsikia ndugu fulani, wakati mmoja, akitumia kifungu hiki. Ndipo niliwazia. . . Nilikiandika. Nikawazia, "Vema, ninaamini nitaandika hicho, maana huenda kikasaidia."

Mara nyingi tunafanya jambo hilo. Ninaona, wengi wenu hapa, walikuwa na kipande cha karatasi. Na mhudumu anaweza kuwa anasema jambo fulani, halafu wewe uta—utashika jambo hilo, kitu fulani kitakugusa ndani yako. Na halafu kama Roho Mtakatifu anafanya hivyo, basi utaanza kujenga kutoka mahali papo hapo, ujumbe wa Bwana. Na hilo ni sawa. Nimeona katika mikutano, popote uendapo, wahubiri tu na watu wakiandika. Hilo ni sawa. Tu—tupo hapa, hilo ndilo lililotuleta hapa, ni kujaribu kusaidiana mmoja kwa mwingine kwenye barabara hizi.

33 Na sasa hebu tufungue Ufunuo, mlango wa 3, kwenye nyakati za kanisa, kurudia wakati wa kanisa. Lakini sasa tunaninii. . . tuna. . . pale. Naam. Ningeweza kuchukua fungu hili moja la maneno, na kwa Roho Mtakatifu, nihubiri juu Yake miaka mia moja na wala nisiweze kutoa kilicho ndani Yake. Kwa sababu, katika fungu hili moja la maneno, kama mafungu mengine yote ya Biblia, yote yamefungwa pamoja.

Nami ninataka kuchukua somo langu, asubuhi ya leo, juu ya hili: *Ninawezaje Kushinda?* Sasa, nilichagua hili kwa sababu ninafikiri ni wakati ambapo hatupaswi kuacha Roho ya uamsho ife. Inatupasa tudumu katika uamsho, tuhuishwe daima, kila siku. Paulo alisema ilimbidi "kufa kila siku, kusudi Kristo aweze kuishi." Wala haitupasi kuacha ufufuo huo ufe, ndani yetu.

Sasa, Ufunuo, mlango wa 3, na kuanzia na kifungu cha 21, tunasoma hivi.

> *Yeye ashindaye, nitampa kuketi pamoja nami katika kiti changu cha enzi, kama mimi*. . . nilivyoshinda *nikaketi pamoja na baba yangu katika kiti chake cha enzi.*
>
> *Yeye aliye na sikio, na alisikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa.*

34 Je! mliona lile—lile 'pangilio la jambo hilo? Unaona? "Kuketi pamoja nami *katika* kiti Changu cha enzi," si "*juu ya* kiti Changu cha enzi." "*Katika* kiti Changu cha enzi," hiyo ni katika milki Yake. Unaona? Na hapo, kwa—kwa kuwa Kristo ndiye Mtawala, Mtawala wa kiti cha enzi wakati huu, wa milki nzima ya Mungu, ndivyo Kanisa litakavyokuwa pamoja Naye, Bibi-arusi atakavyokuwa pamoja Naye, katika kiti Chake cha enzi, katika milki yote. Unaona? Si "*juu ya* kiti Changu cha enzi," bali "*katika* kiti Changu cha enzi," unaona, ambako milki Yake inafika. Kiti cha enzi kinatawala milki, na—na milki inaishia tu

mahali mipaka yake inapoishia. Na hii ni tangu Umilele mpaka Umilele. Wazia tu juu ya jambo hilo!

35 Sasa, tunaposoma hili, kusudi langu la jambo hili si kuja tu hapa ku—kushiriki pamoja na ninyi watu. Jambo ambalo, ninapenda kufanya. Lakini kama—kama ningalikuwa na nafasi ya kufanya jambo hilo, ningalikuja nyumbani kwenu, na kuwapa mkono na kuzungumza nanyi, na kuketi chini, nile chakula cha jioni pamoja nanyi; na kuketi chini, chini ya mti wenye kivuli, na kuzungumza na kushiriki kidogo.

Lakini tunapokuja hapa, tupo hapa kwa ajili ya kusudi moja maalum. Hii ni nyumba ya masahihisho. Hiki ni kiti cha enzi. Hiki ni kiti cha enzi cha Mungu, na hukumu hutoka katika nyumba ya Mungu. Na hapa ndipo tunapokuja pamoja, tunakusanyika katika upendo, mmoja kwa mwingine, kwa kuwa Wakristo tu ndio wanaoweza kupenda. Lakini, hapa ndani, tuko—tuko chini ya u—u—u—uongozi wa Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu yuko miongoni mwetu. Nasi tupo hapa kuwa... kuchukua hesabu miongoni mwetu, kuona mahali ambapo tumepungukiwa, unyonge wetu, na jinsi tunavyoweza kufikia mahali tunapopaswa kuwa, kufikia mahali tunapopaswa kuwa sasa; mahali tulipo, na mahali tunapopaswa kuwa. Na hayo ndiyo tunayojifunza. Wahudumu hujifunza sehemu hizo, kwa ajili ya watu wao. Wanapowaona watu, wanakopungukiwa, basi wanaanzia kwenye hilo.

36 Sasa, hivi karibuni, nafikiri ya kwamba kanisa labda linapaswa kuwa likichukua hatua ndogo kupanda juu zaidi wakati huu. Sikusudii kufanya hivyo asubuhi ya leo, kuwaonyesha mambo haya. Lakini na—nafikiri, baadaye kidogo, Bwana akipenda, kabla hatujahubiri juu ya hizo Baragumu, ninataka ku—ku—kulileteа Kanisa kitu fulani tu ambacho—ambacho mnapaswa kujua, ninaamini, sasa.

37 Na sasa tunazungumza juu ya jambo hili, "kushinda." Neno *kushinda*, hakika, mnajua kile linachomaanisha. Inakupasa kuwa na kitu cha kushinda. Na wakati huu wa kanisa ambao Roho Mtakatifu alikuwa akinena habari zake hapa, kwenye Wakati wa Kanisa la Laodikia, kama vile ambavyo tumeupitia hivi punde, ulipaswa kukemewa. Laodikia ulipaswa kukemewa, kwa sababu ya ku—kutomjali Kristo. Ulikuwa umemweka Kristo nje, katika—katika wakati wao. Na Kristo alikuwa nje, akijaribu kurudi ndani. Huo ni upendo. Baada ya Yeye kutupwa nje ya nyumba Yake Mwenyewe, alikuwa akijaribu kurudi ndani, na akasema, "Yeye atakayeufungua mlango, nitaingia nije kwake." Unaona? Kanisa, lenyewe, kwa jumla, lilikuwa limemtupa nje.

38 Lakini sasa angalieni. Wito wake hapa sio kwa kanisa tu. "Yeye ashindaye." Unaona? Sio kanisa; hilo lingekuwa ni mke,

unaona, mwili wa kanisa. Lakini ni "yeye ashindaye," mtu binafsi atakayeshinda, sasa.

39 Na Laodikia ulikuwa nao ukimjia. Sasa tunaona, basi, tukijua ya kwamba huu ndio Wakati wa Laodikia, na tukijua ya kwamba wakati huu unahitaji kukaripiwa vikali na Mungu. Unapaswa kukaripiwa vikali. Na makasisi wetu wanapokuwa wanyonge sana na wazembe, kama babu mwenye umri mkubwa kwa wajukuu wake, yote wafanyayo ni makamilifu. Nao wananinii . . .

40 Imesemwa sana, ya kwamba Mungu ni Mungu mwema sana, mpaka wanajaribu kumfanya Mungu babu mkubwa mzembe. Mnaona? Lakini sivyo alivyo. Yeye ni Baba, na ni Baba wa haki, wa marudio. Na upendo daima husahihisha. Unaona? Upendo husahihisha. Haidhuru unaumiza jinsi gani, ungali unasahihisha.

Mama halisi atawarudi watoto wake. Baba halisi atawarudi. Unaona? Kama ukiwa tu debwedebwe na mzembe, na kuachilia ninii . . .

41 Nilikuwa nikivuka gogo lililochakaa hivi majuzi, kushuka kwenye ki—kijito, ama kinachoitwa bonde. Nami nikaruka juu ya gogo hili. Kwa nje, lilionekana ni zuri, lilionekana kama gogo kubwa lililochakaa la mti wa bichi. Lakini nilipolirukia, loo, kipande kikubwa chake kilianguka. Kilikuwa kimeoza kabisa na kuchakaa. Nikasema, "Hivyo ndivyo Wakristo wanavyokuwa." Wamekwisha kufa katika dhambi na maovu, kwa muda mrefu sana, hata wamevunda. Hawawezi kustahimili uzito wowote, hata kidogo. Ha—hawajui maana ya kushinda. Ndipo nikaanza kuwazia juu ya somo hili, wakati huo. Kushinda, kudumisha Uzima ndani yako. Wakati uhai ulipotoka, hilo ndilo lililosababisha gogo hilo kuwa katika hali hiyo. Unaona? Na ilifanya hali yake kuwa mbaya zaidi kuliko wakati lilipokaa kwenye tawi ambako kulikuwa na maji.

42 Halafu basi, hapo, ukimchukua Mkristo, ambaye anadhaniwa kuwa Mkristo, acha Uzima wa Mungu umtoke, na ule ujuzi, ile furaha ya kumtumikia Kristo; na, akiishi kwenye kanisa ambako mambo haya yanaendelea, ataoza upesi maradufu, kweli, akiishi moja kwa moja chini yake.

43 Kwa hiyo, kama tunajaribu kuufuata Ujumbe wa wakati huu, ama angalau sehemu hii ya Ujumbe, inatupasa kuishi daima katika maisha ya Kristo. Unaona? Maana, tusipoishi, ukikaa hivyo, na kujua Hayo, mambo haya unayopaswa kufanya, wala huyafanyi. Biblia ilisema, "Yeye ajuaye kutenda mema, wala hayatendi, kwake ni dhambi." Ndipo unakuwa mzembe, umeoza, unapotengwa na Uzima wa Mungu. Kwa hiyo, jitahidi kwa yote yaliyo ndani yako, kudumu katika Uzima wa Kristo, upate kuzaa matunda.

44 Tunaona wakati huu tunaoishi. Ni mmoja wa nyakati nzuri sana za nyakati zote. Wakati huu wa Kanisa la Laodikia ndio mzuri sana kuliko nyakati zote za kanisa, kwa maana ni mwisho wa wakati na kuungana kwa Umilele. Na, basi, ndio wakati ulio mkuu sana wa dhambi. Kuna dhambi nyingi zaidi katika wakati huu kuliko zilizopata kuwapo. Na nguvu za Shetani ni—ni ngumu zaidi kupigana nazo kuliko ilivyokuwa katika wakati wowote. Unaona? Hapa!

45 Huko nyuma katika nyakati za mwanzoni, Mkristo angaliweza, kwa ushuhuda wake wa kuwa ninii wa kanisa . . . wa kuwa yeye ni wa Kristo, angeweza kukatwa kichwa kwa sababu hiyo. Angeweza kuuawa, na kuondolewa kwenye shida zake, na aende kukutana na Mungu, upesi.

Lakini sasa adui ameingia, katika jina la kanisa, naye ni mdanganyifu sana. Huu ndio wakati mkuu sana wa udanganyifu. Wakati, Kristo alisema hivyo, "Roho hizo mbili zitafanana sana katika siku za mwisho hata zingewadanganya walio Wateule kama yamkini." Unaona? Unaona? Unaona? Kumbukeni, Kristo alizungumza juu ya watu fulani walioteuliwa kwa ajili ya siku za mwisho. Mnaona? "Ingewadanganya walio Wateule kama yamkini." Kufanana sana! Watu waishi hivyo, watu wanaweza kuishi maisha safi, matakatifu; wasiwe watenda dhambi, wazinzi, na walevi, na wadanganyifu, wacheza kamari. Wanaweza kuyaacha hayo, na bado wasiwe Naye. Hiyo ni kweli.

46 Huu ndio wa—wakati wa Uhai, Uhai binafsi wa Kristo, ambapo, ke—kemia ya Mwili Wake, kile kilichokuwa ndani Yake.

Kwanza, chini ya kuhesabiwa haki, ubatizo wa maji. Pili, chini ya Kuzaliwa kupya, kwa Wesley, kutakaswa, ambako hutakasa. Na ya tatu, chini ya ubatizo wa Roho Mtakatifu, kukiweka kazini hicho chombo kilichotakaswa. Unaona? Neno *kutakasa* linamaanisha, ni neno la Kiyunani lenye sehemu mbili ambalo linamaanisha "kusafishwa na kutengwa kwa ajili ya matumizi," kutengwa kwa ajili ya matumizi. Sasa Roho Mtakatifu hukiweka katika matumizi. Unaona?

47 Nasi tutaona, "Roho mchafu amtokapo mtu, hupitia mahali pasipo maji." Hivyo ndivyo kanisa limefanya hasa, Wabaptisti, Wamethodisti, hao walioamini katika utakaso. "Kisha," Yesu alisema, "pepo mchafu aliyetoka, anarudi kwenye mwili huu wa kanisa na kukuta nyumba iliyopambwa, ikafagiwa ikawa safi sana, inaishi maisha safi, yasiyo na hatia." Vema. "Lakini basi kama nyumba hiyo haijajazwa, ikakaliwa, ndipo anaingia na pepo wengine saba waovu walio wabaya kuliko alivyokuwa yeye, na hali ya mwisho ya mahali hapa ni mbaya mara saba kuliko ilivyokuwa mara ya kwanza." Ilikuwa ni bora wao kukaa wakiwa Walutheri, kuliko ambavyo ingekuwa kupokea hiyo Nuru na

kushindwa kuifuata. Ndivyo itakavyokuwa kwa Wapentekoste, unaona, unajua ninalomaanisha, nyumba imepambwa.

48 Kama nilivyokuwa nikizungumza na mtu mmoja, hivi majuzi, kasema, "Wao ni waangalifu sana, hata wengi wa makundi ya utakatifu, kutomwita Roho Mtakatifu, '*Holy Ghost*,' maana wanajitambulisha na Wapentekoste wanapofanya hivyo. Wanasema, "*Holy Spirit*," unaona, wasije wakasema, '*Holy Ghost*.'" Kwa sababu, Wapentekoste, watu wa kawaida, wanamwita tu vile Biblia inavyosema, "*Holy Ghost*." Ambapo, *Holy Spirit* na *Holy Ghost* ni kitu kile kile. Bali wao ni waangalifu sana kuhusu jambo hilo. Hawataki kujitambulisha na hao watu wanaonena kwa lugha; na huyo ni Roho Mtakatifu, Mwenyewe. Unaona?

Ni nini kilitukia basi? Wakati adui, aliyetoka akaenda chini ya utakaso, aliyekuwa ameoshwa, aliporudi na kukuta nyumba haijajazwa na Roho Mtakatifu, sasa hali ya kanisa imeungana na—na shirika la makanisa, na Baraza la Makanisa Ulimwenguni. Na ni hali sasa inayowaunganisha na Ukatoliki wa Kirumi na hayo mengine yote, na sasa limekuwa baya mara saba kuliko lilivyokuwa wakati lilipotoka katika Ulutheri. Huko ndiko mwanadamu anakolipeleka.

49 Halafu basi angalia Wakati wa Kanisa la Laodikia baada ya kumpokea Roho Mtakatifu, na pamoja na maarifa na Roho wa Mungu ndani Yake, na halafu kazi za Mungu zinakanushwa nalo, na kuiita "kazi chafu." Basi vipi kuhusu jambo hilo? Hapo ndipo Kristo anapotolewa katika kanisa Lake Mwenyewe. Unaona? Yeye . . . Halikumwonyesha Yeye akiwa kanisani mpaka ilipofikia kwenye Laodikia; na wakati alipofika Laodikia, alikuwa ametolewa kanisani Mwake, akijaribu kurudi ndani.

50 Sasa, unaona, kuhesabiwa haki kamwe hakukumwingiza ndani. Utakaso ulipasafisha tu mahali hapo kwa ajili Yake. Bali wakati ubatizo wa Roho Mtakatifu ulipokuja, ulimweka ndani ya watu. Na sasa wao walimfukuza, wakati alipoanza kujionyesha Mwenyewe, kwamba ni Yeye yule jana, leo, na hata milele. Walimfukuza kwa sababu wameunda madhehebu, na Ro—Roho wa Bwana hakubaliani na madhehebu yao. Mnafahamu sasa? [Makusanyiko yanasema, "Amina."—Mh.] Kwamba, walimweka Yeye nje. "Hatutaki uhusiano wowote na telepathia hii. Ni—ni ya ibilisi. Ni upiga ramli. Ama . . . " Unaona?

Hawafahamu. "Macho, wala hawawezi kuona; masikio, wala hawawezi kusikia." Unaona? Mungu huyafungua tu macho anavyotaka Yeye. "Yeye huwafanya wagumu wale anaotaka kuwafanya wagumu, anaotaka kuwafanya, na—na—na anawapa Uzima wale anaotaka kuwapa." Hivyo ndivyo Maandiko yalivyosema.

51 Sasa, tunaona saa hizi tunazoishi, kiwango hiki, na tunaona kwamba ilikuwa ni kitu gani. Na Roho Mtakatifu anaukemea wakati uliomtoa nje. Lakini, katika hayo yote, je! mlitambua, "Yeye ashindaye"? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hata katika wakati huo wa kanisa la kilimwengu, mchafu, "Yeye ashindaye."

52 Tunaona hapa ya kwamba Mungu daima amekuwa na washindi. Amekuwa na washindi katika kila wakati. Daima wapo, kila wakati, katika kila wakati ambao umekuwapo duniani, Mungu daima amekuwa na mtu fulani ambaye angeweza kuweka mikono Yake juu yake, kama shahidi duniani. Kamwe hajakuwa bila shahidi, ingawa wakati mwingine ni mmoja tu. Lakini mtu fulani anashinda, sasa, kama watakatifu wale wa kale.

53 Na mtu m—mzuri sana, msomi, alikuwa akisema, baada ya *Ile Mihuri Saba*, yeye alisema, "Ndugu Branham, kwa kuwa wewe ni m—mfananishi, ni mwenye kuainisha, hasa," kasema, "utawezaje kuweka Kanisa hilo katika Unyakuo pasipo ule wakati wa Dhiki, katika mfano?" Akasema . . .

Unaona, kama ni mfano, hapana budi kuweko na . . . hakuna budi kuweko . . . Kama kuna mfano wa kufananishia, hapana budi kuweko na mfano utakaotoka kwenye huo mfano wa kufananishia. Na kila kitu ninachosema, ambacho ni kweli, kina mfano wake. Kina mfano wake. Una kivuli. Nayo Biblia ilisema, "Mambo ya kale yalikuwa ni mfano wa mambo mapya yatakayokuja."

Yeye alisema, "Lakini sasa ulichukua Agano la Kale kama mfano. Sasa," akasema, "utafanyaje na Kanisa hili?"

54 Mtu huyu anatoka kwenye ninii . . . Mtu mkuu, mwalimu mashuhuri ambaye ni rafiki yangu msiri, mtu mkarimu sana, naye ni ndugu mzuri sana. Ni—nisingethubutu kusema neno moja dhidi ya ndugu huyo. Nisingesema, hata hivyo. Kama—kama ninii . . . Kama Mkristo, nisingesema neno dhidi yake. Ha—ha—hakubaliani nami juu ya somo hilo moja, bali ye—yeye ni ndugu yangu wa thamani. Tunakula pamoja. Na, loo, yeye ni jamaa mzuri tu. Mimi huchukua gazeti lake, nasoma makala yake. Naye huandika baadhi ya ya kwangu, na kadhalika. Nami nimechukua masomo mengi kutoka kwenye ya—yale nimesoma—soma ya makala yake, niliyomsikia akisema. Yeye ni mtu mashuhuri, bali ha—hawezi kamwe kukubaliana nami. Ninathamini jambo hilo, kuhusu uaminifu wake. Ingawa yeye haninii tu, mmoja wa hawa wenye kusukumwa kwa urahisi, wenye kukubaliana tu na kila kitu unachosema. Yeye ana ushawishi wake mwenyewe, naye huusimamia. Ninathamini jambo hilo. Naye ni mtu mzuri. Loo, mimi—mimi si mwalimu wala msomi, hata kidogo, bali mtu huyu ni mwalimu na msomi pia.

55 Lakini si—siwezi kukubaliana naye, maana silioni. Lakini, halihusu wokovu, linahusu Kuja kwa Bwana. Yeye anaona ya kwamba Kanisa halina budi kupitia kwenye wakati wa ile Dhiki, kwa ajili ya kusafishwa. Mimi ninasema Damu ya Yesu Kristo ililisafisha Kanisa. Unaona? Halihitaji ninii . . .

Ninaamini ya kwamba kanisa linapitia katika wakati wa ile Dhiki, kanisa la kidhehebu, bali Bibi-arusi hapitii. Je! ungemchagua mwanamke ambaye ilikubidi kumsafisha kabla ya wewe kumwoa? Unaona? Bibi-arusi wa Kristo amechaguliwa, pia ni Mteule. Naye ni Bibi-arusi wa Mungu, Bibi-arusi wa Yesu Kristo.

56 Na sasa yeye alisema, “Utafananishaje hilo, kama huyo Bibi-arusi akiondoka, akiondoka kabla ya kupitia kwenye ule wakati wa Dhiki?” Kasema, “Nina Maandiko yanayokuonyesha ya kwamba Kanisa liko katika wakati wa ile Dhiki.”

Nikasema, “Hebu soma tu Mhuri wa Sita, hivyo tu, yeye yuko moja kwa moja pale chini ya wakati wa ile Dhiki. Lakini tunaona, kabla tu ya jambo hilo, Bibi-arusi amekwisha kwenda. Unaona? Yeye yuko Utukufuni wakati huo. Hana kutakaswa.” Unaona?

“Yeye aniaminiye Mimi yuna Uzima wa milele, wala hataingia hukumuni ama kwenye ile Hukumu, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani.” Kristo alitoa ahadi ya kwamba hata tusingesimama Hukumuni. Yeye alipachukua mahali pangu kwa hiari Yake, mpaka mimi ni huru kabisa. Ninaposamehewa, nimesamehewa. Anawezaje kunitoa katika duka la rehani, nina risiti dhahiri, kama . . . Anawezaje kuwa Mkombozi wangu, na kunitoa kwenye duka la rehani, kisha dalali aendelee kusema mimi ni mali yake? Ninayo risiti iliyoandikwa, amina, unaona, iliyoandikwa kwa Damu ya Yesu Kristo. Unaona? Sasa, katika jambo hilo, hapa ndipo tulipofikia.

Yeye alisema, “Sasa, utapataje, kumtenganisha huyo Bibi-arusi mteule unayenena habari zake sasa, utamwekaje Huyo chini ya mfano?”

57 Nikasema, “Vizuri kabisa.” Nasema, “Hili hapa. Sasa, katika Mathayo, mlango wa 27 na kifungu cha 51.” Kama tukininii . . .

Hebu nilisome tu, na ndipo tu—tutalipata vizuri. Ndipo tutaona kama ilionyeshwa kwa mfano ama haikuonyeshwa, kama ni Bibi-arusi aliyeteuliwa. Mathayo, mlango wa 27 na ki—na kifungu cha 51. Vema. Tunasoma hivi, kwenye kule kusulubiwa kwa Bwana wetu.

> *Na tazama, pazia la hekalu likapasuka vipande viwili toka juu hata chini;* . . .

58 Sasa, hiyo ilikuwa ni torati. Torati ilikomea papo hapo. Kwa sababu, lile pazia lilitenga kusanyiko na vitu vitakatifu vya Mungu. Ni kuhani aliyetiwa mafuta peke yake aliyeingia mle,

na, hilo, mara moja kwa mwaka. Mnakumbuka? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Sasa, Mungu, kwa mkono Wake Mwenyewe, angalieni, "toka juu hata chini," si toka chini mpaka juu. Ni kadiri ya futi arobaini kwenda juu. Angalieni, si toka chini mpaka juu, bali ni "toka juu mpaka chini," ilionyesha hilo lilitendwa na Mungu. Akapasua pazia vipande viwili, ndipo hata hivyo, yeyote yule, yeyote atakaye, anaweza kuja na kushiriki utakatifu Wake. Unaona? Vema.

> *. . .kutoka juu hata chini; nchi ikatetemeka; miamba ikapasuka;*
>
> *Makaburi yakafunuka, ikainuka miili mingi ya watakatifu waliolala;*
>
> *Nao wakiisha kutoka makaburini mwao, baada ya kufufuka kwake. . .wakaingia mji mtakatifu wakawatokea wengi.*

59 Huyo hapo yule Mteule, yule Bibi-arusi. Si kanisa lote la Kiyahudi lilitokea wakati huo. Wote walitoa dhabihu ile ile. Wote walikuwa chini ya damu iliyomwagika ya mwana-kondoo. Bali kulikuwa na Kundi lililoteuliwa; na Kundi hilo lililoteuliwa, mara tu tukio hilo lilipotukia, hilo lililiamini kwa uaminifu kweli. Sasa ninalifikia neno *kushinda*. Sasa shikilia hilo. Hawa ambao walikuwa wameshinda kweli, wakitoa dhabihu ile ile kwa uaminifu ambayo wengine wao waliitoa, lakini, katika uaminifu, waliyashinda mambo ya ulimwengu. Wakati upatanisho ulipofanywa vizuri kwa ajili yao, walikuwa paradiso mpaka kwenye tukio hilo wakati huo. Wakati huo ulipotimia, walikuwa wameshinda na walikuwa wakipumzika, wakilala; unaona, "miili mingi ya wale waliolala mavumbini," unaona, waliolala.

60 Sasa, kama tungalikuwa na wakati, tungalirudi kwa Danieli, wakati, Danieli, yule mteule aliyekuwa ameshinda. Naye alisema, "Kifunge Kitabu, Danieli, maana utapumzika katika kura yako. Lakini wakati Jemadari atakapokuja, atakayesimama upande wa hao watu, wewe utasimama katika kura hiyo." Huu hapa. Danieli, nabii huyu wa Mungu, aliona wakati wa mwisho ukija. Naye alisema, "Danieli, utasimama katika kura yako kwenye siku hiyo." Naye huyu hapa, akatokea; sio Israeli wote, bali Israeli mfano wa Bibi-arusi. Sasa, hao Israeli wengine hawatokei mpaka kwenye ufufuo wa kiama.

61 Na sasa, kwenye kule Kuja kwa Bwana Yesu, wale ambao kweli wanakupenda Kuja Kwake, wanaoishi kwa kuungojea huo; wakati atakapotokea angani, Kanisa lililolala mauti katika Kristo litafufuka, na hao watabadilishwa katika kufumba na kufumbua. Hao wengine hawatajua kitu juu yake. Kumbukeni, "Wakawatokea waliokuwa mjini." Unaona? U—U—Unyakuo utakuwa hivyo. Tunaonana mmoja kwa mwingine, na tutawaona. Walimwengu waliosalia hawatawaona.

Tutanyakuliwa kama kuondoka kisiri. Tunaungojea wakati huo!

Ndipo kurudi duniani kwa ajili ya ule Utawala wa fahari wa Miaka Elfu, ndipo ile miaka elfu . . . "Hao wafu waliosalia hawakuwa hai hata itimie ile miaka elfu moja."

62 Ndipo unakuja ufufuo wa kiama, ambapo, Israeli wote. Na pia, angalieni hapo, wale mitume kumi na wawili, wale wazee wetu kumi na wawili, wote wanawakilishwa. Na hata hatujafikia jambo hilo bado. Pengine, Bwana akipenda, tutalifikia kwenye Agano, jinsi ambavyo hizo kuta za yaspi, na yale mawe kumi na mawili, milango kumi na miwili, misingi kumi na miwili, hizo zote zimewakilishwa. Hawa hapa juu ya viti kumi na viwili vya enzi, wale malaika wajumbe wa siku hizo, kutoa hukumu juu ya wale walioukataa ujumbe wao. Amina. Hiyo hapo ile saa kuu inakuja. Naam.

63 Ni siku ya namna gani, ni wakati wa jinsi gani tunaoishi! Jinsi ambavyo inatupasa kujichunguza, Kanisa. Sasa tunazungumza juu ya mambo haya yanayokuja, yatakayokuja. Sasa, leo, hebu turudi hapa na tuone, tujichunguze wenyewe tuone kama tuko kabisa katika Imani.

64 Sasa hebu tuzungumze juu ya washindi wachache kwa dakika chache, katika siku za Nuhu, ambao ulifananishwa na Yesu Kristo, kwamba ni kama wa leo hii.

Ninapaswa kuwa na dakika kumi. Sasa nitachukua nusu saa. Ndiyo kwanza ninaanza, ukurusa wa kwanza. Nitaruka chache, nikiweza. Na kupata kile . . .

65 Katika wakati wa Nuhu, mfano wa siku hizi: Yesu aliurejea, na kusema, "Kama ilivyokuwa katika wakati wa Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika Kuja Kwake Mwana wa Adamu. Katika wakati wa Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika Kuja Kwake Mwana wa Adamu." Angalia, kulikuwako na ulimwengu huo wote ulioitangulia ile gharika, labda wa mamilioni ya watu, kulikuwa na washindi wanane. Watu wanane walishinda, ambao walikuwa ni washindi halisi, wa kweli. Kulikuwako na wana watatu wa Nuhu pamoja na wake zao, na Nuhu na mke wake. Wanane walishinda, walioingia kwenye safina wakati uliofaa. Waliifanyaje? Walilisikiliza Neno la Mungu. Hawakupatikana nje ya mlango. Walipatikana ndani ya mlango.

66 Loo, jamani rafiki zangu wapendwa, msiache mlango huo ufungwe. Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku hiyo, ndivyo itakavyokuwa katika Kuja Kwake Mwana wa Adamu." (Asante, ndugu.) "Ndivyo itakavyokuwa katika Kuja Kwake Mwana wa Adamu." Sasa, yupo mtu atakayepatikana akiwa nje ya mlango huo.

Wengi wao huenda walikuwa na nia njema, na, "Siku moja, kama mambo kama hayo yakitukia, tutaingia pamoja na Ndugu

Nuhu, maana yeye ni mtu mzuri." Lakini, unaona, ni wanane tu waliopatikana wakiwa ndani.

67 Sasa, wazia sana sasa. Kama umekaa vivi hivi, ukiwa mzembe, ingia. Hima, upesi, maana mlango huenda ukafungwa wakati wowote.

68 Na daima kumekuwa na safina katika uchumi wa Mungu. Kulikuwa na safina katika siku za Nuhu, kwa ajili ya kuwaokoa watu Wake. Kulikuwako na safina katika siku za torati, sanduku la ushuhuda. Katika siku za torati, walilifuata lile sanduku la agano.

Na kuna kipindi cha tatu cha wakati sasa; kama kwenye wakati wa Nuhu, wakati wa Lutu, halafu sasa wakati huu. Kuna safina sasa. Na safina hiyo si dhehebu, wala si matendo mema unayotenda. Ni "kwa Roho mmoja," Warumi 8:1, "sote tumebatizwa katika Mwili mmoja, katika milki ya ule Ufalme, ubatizo mmoja wa Kiroho." Haidhuru wewe ni mzuri jinsi gani, ni mbaya jinsi gani, chochote kile, uko katika Ufalme huo kwa—kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Unaona? Hivyo ndivyo tu unavyoshinda. Ni wale wote walio chini ya ile Damu iliyomwagika ndio washindi, maana huwezi kushinda, wewe mwenyewe. Yeye Ndiye anayekushindia. Wewe unapumzika.

69 "Nitajuaje basi, Ndugu Branham, ya kwamba mimi nimo Mle ndani?" Angalia ni maisha ya jinsi gani unayoishi. Angalia tu kote. Angalia kama yanaishiwa tu kutoka kwako, bila jitihada zako. Ama, inakubidi kujitahidi na kuvuta, unaona, basi wewe ndiwe unayejiishia. Lakini usijaribu kuyaishi. Je! uliwahi kujaribu? Naam. Usijaribu.

70 Ni kama tu kuweka mkono mdogo wa mtoto kuuingiza katika mkono wa vazi, unaona. Yeye anarukaruka tu juu, chini, juu, na chochote kile. Unaona? Hawezi kufanya hivyo. "Vaa koti lako, kipenzi." Hawezi kulivaa. Mkono mdogo uko juu, chini, kote. Inahitaji mkono wako uliotulia.

Loo, jinsi nilivyo na furaha, ninaweza tu kuutoa mkono wangu kwa Baba, niseme, "Bwana Yesu, siwezi kuingia Mle. Nisaidie. Nivalishe koti." Ninaacha kujaribu. Nimwache tu anivalishe. Unaona?

71 Kama mtoto huyo mdogo akiendelea kujaribu, "Loo, ninaweza kujivalisha. Ninaweza kujivalisha." Naye anaingiza tu kila mahali. Hawezi kujivalisha.

Wala nawe huwezi, wala mimi siwezi, bali kama tutatulia tu na kumwacha afanye hivyo. Jisalimishe tu Kwake, "Hapa, Bwana, mimi hapa. Ja—jalia tu nisiwe kitu. Na—najisalimisha. Weka mkono wangu mahali sahihi." Huo ndio ushindi. Huko ndiko kushinda.

72 Kitu unachopaswa kushinda ni wewe mwenyewe, wazo lako, kitu chako, na ujisalimishe mwenyewe Kwake. Yeye alikushindia. Yeye anajua njia; sisi hatuijui.

73 Lakini katika wakati wa Nuhu kulikuwa na washindi wanane, na hao ndio walioingia. Walikutwa wakiwa ndani.

Sasa angalieni, enyi marafiki. Ninaamini wanaurekodi huu. Na kama uko kwenye televisheni, ama si tele-. . . samahani, kanda. Chochote ufanyacho, wewe ambaye unasikiliza sasa, ama yeye atakayesikiliza baadaye, saa imeenda sana, nawe una makusudi mema, lakini hebu ukutwe ndani. Sasa, usijitahidi. "Si yeye atakaye, wala yeye apigaye mbio, bali ni Mungu." Mruhusu tu Mungu. Jisalimishe tu Kwake na uendelee kutembea, kwa imani kamilifu, iliyoridhika, ya kwamba, "Yale Mungu ameahidi anaweza kuyatimiza." Sio kujiunga na dhehebu moja, dhehebu lingine, kukimbia *huku*, *kule*, ama kule *kwingine*, ukijaribu *hili*. Jitoe tu kwa Mungu, na utembee pamoja Naye, umejaa amani, mtulivu, bila kupingwa. Endelea tu kutembea pamoja Naye. Hiyo ni kweli.

74 Hivyo ndivyo nilivyomwambia ndugu yetu ambaye ndiyo kwanza a—apoteze fahamu. Unaona? "Jisalimishe tu Kwake. Yeye yupo hapa, Yeye aliyejua yale uliyofanya, na kile kilichosababisha uwe hivi na kufanya *hivi*, na yote hayo. Yeye anajua yote kukuhusu wewe, na sasa Yeye amekwambia tu la kufanya. Sasa," nikasema, "jambo pekee unalopaswa kufanya ni kwenda tu kulifanya. Hiyo ni kusema, sahau yote yaliyopita, tembea, ishi kwa ajili ya siku za usoni, katika Utukufu na Uwepo wa Mungu."

Washindi wanane.

75 Katika siku za wakati wa Danieli, kulikuwa na washindi wanne ambao waliweza kustahimili jaribio la moto na simba.

Sasa, tunatarajiwa kujaribiwa. Hilo ni somo zuri kwa ndugu ya—yangu hapo nyuma, pia. "Yeye amjiaye Mungu hana budi kujaribiwa kwanza." Kujaribiwa (nini?) kwa Neno. Hilo ndilo jaribio la Mungu. Je! mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] "Yeye amjiaye Mungu hana budi kujaribiwa." Hiyo inaonyesha tu mtoto wa kweli, basi, unaona, kujaribiwa. Na wakati jaribio linapokuja. . . Huwezi kushinda usipopewa jaribio. Na jaribio likitolewa, ni kuona kama unaweza kushinda ama huwezi. Na Yesu alisema, "Yeye ashindaye," lile jaribio. Jaribio ndilo jambo kubwa sana lililowahi kukupata. Ninaamini imeandikwa katika Maandiko, Petro alisema, ya kwamba, "Kujaribiwa kwetu kuna thamani kuu kwetu kuliko dhahabu yenye thamani." Ni wakati wa kujaribiwa. Ni thibitisho moja zuri kwetu kwamba Mungu yupo pamoja nasi, tunapojaribiwa, kwa kuwa watoto wote wa Mungu wanajaribiwa na kupimwa.

76 Basi Danieli, mwanadamu, nabii; Shadraka; Meshaki; na Abednego; Danieli ndiye aliyekuwa nabii; na huo ulikuwa ndio ukubwa wa Kanisa katika siku hiyo, ninamaanisha, Bibi-arusi. Kuna wafuasi wengi sana wa kanisa, karibu milioni mbili wa hao walishuka wakaenda kule. Lakini kulikuwa . . . Hiyo ndiyo iliyokuwa idadi ya washindi. Na hao washindi walijaribiwa. Na kila mshindi hana budi kuwekwa kwenye kujaribiwa. Na waliposema, "Ninyi ghairini yale Neno lisemayo, la sivyo mtatupwa kwenye tanuru la moto," wao walikataa kitu chochote ila Neno.

77 Na wakati Danieli alipojaribiwa, ya kwamba aghairi yale Neno liliyosema, ya kwamba inawapasa kuegemea kwenye hekalu, kama vile Sulemani alivyoomba, naye angewakomboa na mambo yote. Mungu angesikia kutoka Mbinguni kama wangekaa . . . wangeelekea kwenye hekalu na kuomba. Ndipo akasema, "Kama mtu yeyote akiomba katika kipindi cha siku hizi . . . Nasi ni Wamedi-Waajemi, ambao hatuwezi kugeuza wala kubadili sheria zetu. Mtu huyo atatupwa kwenye tundu la simba."

78 Walimwekea mtego. Ninaamini ya kwamba nabii huyo alijua jambo hilo. Bali walimwekea mtego. Alitembea kwa unyenyekevu. Wakati wake wa kuomba ulipowadia . . . Wakati, yeye alijua, huko nyumbani Yerusalemu, kulikuwako na dhabihu ya kuteketezwa madhabahuni. Danieli hakuwaogopa hao wapelelezi. Alifungua pazia, na akafungua madirisha, kisha akapiga magoti yake, na kumwinulia Mungu mikono yake na kuomba. Kwa nini? Aishi ama afe, yeye alikuwa na ushindi. Na, kwa hiyo, ushindi mwingi sana hata simba hawakuweza kumla. A—alishinda.

79 Hao . . . Shadraka, Meshaki, Abednego walikuwa na ushindi mwingi sana hata simba . . . hata moto usingeweza kuwachoma. Mnajua, ushindi ni kitu kigumu kuunguza, ama kuliwa, ama chochote kile. Unaona? Kwa hiyo, wao, walikuwa nao.

80 Huenda nikamtaja mtu mwingine. Katika siku za Lutu, Yesu alilirejea hilo, kulikuwako na watatu tu walioshinda, Lutu na binti zake wawili. Si hata mke wake; hakushinda. A—alianza safari. Yeye ni mfano. Laiti tungalikuwa na wakati. Dakika zangu thelathini zimekwisha sasa hivi. Unaona? Unaona? Yeye, alifanya vema, aliondoka.

81 Sasa inanibidi kuwapa jambo hili, kwa muda kidogo tu. Wengi wenu mmeondoka, pia. Wengi wenu mliacha mambo haya, mpate kuchukua msimamo wenu, baada ya kulichunguza kote katika Maandiko na kuona kwamba ni kweli. Mliona thibitisho la Mwenyezi Mungu; si kwa ninii fulani, yale mtu fulani *aliyosema* yalikuwa ni thibitisho. Yale Biblia iliyosema yangekuwa, na hapa yanatukia. Mliona kwamba Hiyo ilikuwa ni Kweli. Kwa hiyo, mmeanza kutoka, kuondoka Sodoma, kuliacha

dhehebu, kuyaacha mambo yanayowafunga kwenye kanuni ya imani; na kumfuata Kristo, kwa Roho Mtakatifu akijithibitisha Mwenyewe kwa Neno la Mungu lililoandikwa. Kwa maneno mengine, mlichukua Biblia badala ya kanuni ya imani. Mlianza kutoka, kufuata.

82 Vema, mke wa Lutu alifanya jambo lile lile, mwajua. Alitoka, apate kwenda pamoja na Lutu, kumfuata mumewe, watoto wake, wapendwa wake, bali halikuwa moyoni mwake. Angali aliipenda dunia. Kwa hiyo inawezekana unaweza kuanza, na bado dunia ingali iwe ndani yako. Unaona? Yeye kamwe hakushinda. Na hata ingawa alikuwa ameendelea sana na safari, hatimaye ilimtupa. Ilimbidi kutupia jicho hilo kubwa, refu, la mwisho. Hapo ndipo aliponasiwa. Hata usiangalie nyuma. Usiwe na tamaa zozote. Endelea kwenda. Weka nia yako Kalvari na uendelee kwenda ukielekea kwa Kristo. Unaona?

83 Alianza safari, kama mshindi, bali kamwe hakushinda. Loo, aliyaacha madhehebu. Aliyaacha. Alitoka Sodoma, pamoja na Lutu. Lakini alitaka kurudi akanyolewe nywele zake. Mnajua ninalomaanisha. Unaona? Ilimbidi arudi nyuma. Kamwe hakuweza kustahimili ja—jaribio. Ilibidi kuangalia nyuma tena, aone kile hao wengine walikuwa wakifanya. "Loo, unajua, nilikuwa na marafiki wazuri kule chini, hata hivyo. Na, hata hivyo, huenda huu ukawa ni u—uamsho mdogo tu. Sijui kama ungeweza kuwa ni wa kweli ama si wa kweli. Ni—nina neno la mtu huyu tu juu ya jambo hilo, ingawa yeye ni mume wangu. Lakini hata hivyo . . . " Mchungaji wako ni mume wako, tukinena kiroho, unaona. "Sasa, kama ungekuwa ni kweli ama si kweli, sijui mimi. Labda yeye, ufunuo wake haukuwa ni wa kweli."

Basi, kama hujaridhika kikamilifu, hujui vizuri kabisa ya kwamba ni Neno la Mungu, basi—basi huwezi kwenda. Unaona? Unapaswa kujitolea kabisa. Unapaswa kujua. Sio kusema tu, "Vema, ninawaona wengine wakifanya jambo hilo. Ninaona ishara."

84 Unajua, Israeli walianza kutoka, ningeweza kusema jambo lile lile na kuliingiza hapa ndani. Walianza kutoka, watu milioni mbili wenye nguvu, wakaishia wakiwa watu wawili. Kweli. Waliziona kazi za Mungu. Waliona dhihirisho la Roho. Waliona miujiza mikubwa mno ikitendwa kule Misri, na kila kitu, nao wakaanza kutoka. Lakini ha—halikuwa moyoni mwao. Hawakushinda. Walitoka tu. Na Yesu akasema, "Nao waliangamia jangwani," na wamekufa Milele. "Kila mmoja wao amekufa," hiyo inamaanisha utengano wa Milele. Kila mmoja wao aliozea nyikani.

85 Lakini kulikuwa na watu wawili, Yoshua na Kalebu. Na wakati ilipofikia jaribio la kuamua, pingamizi zilikuwa kubwa sana hata walionekana kama panzi kando yao. Yoshua alipaza sauti pamoja na Kalebu, na kusema, "Sisi tunaweza hata

na zaidi kufanya jambo hilo." Kwa nini? "Mungu alisema hivyo." Nao walikuwa washindi. Walishinda. Hao ndio waliopata majaliwa, kutoka katika shirika hilo lote kubwa la watu, kumpeleka Bibi-arusi halisi, aliyeteuliwa katika nchi ya ahadi. Yoshua na Kalebu wakiwa kwenye mstari wa mbele kule nje, kama jemadari wawili, waliwaongoza moja kwa moja hadi mtoni, na wakavuka mto, wakaingia kwenye nchi ya ahadi. Kwa nini? Waliliamini Neno, haidhuru nini.

86 Ndipo, Dathani akainuka. Dathani, hasa, aliinuka, na vivyo hivyo na Kora, nao wakajaribu kusema, "Mtu huyu anajaribu kujiinua juu ya wengine wetu wote; yeye ni mtakatifu kuliko wengine wote." Baada ya Mungu kumthibitisha mtu huyo kwelikweli. Wao walisema, "Tutaanzisha tu kundi la watu na tutaunda *hili*, *lile*, ama *linginelo*, na tutajiundia madhehebu yetu, tutafanya . . . " Nao wakafa na kuangamia.

Lakini watu hao walikuwa na hilo Neno la Bwana, nao wakadumu Nalo, nao wakavuka.

"Si yeye aanzaye; yeye amalizaye." Wengi huanza mbio, bali kuna Mmoja anayeimaliza. Kutakuwako na makanisa mengi yatakayoanza, makundi mengi ya watu. Kutakuwa na Kundi moja litakalomaliza. Hao ndio washindi.

87 Siku za Lutu, naam, ilibidi mke kutupa hilo jicho kubwa refu huko nyuma. "Loo, ninawaacha akina *Nanii* huko chini, hizo nyakati nzuri tulizokuwa nazo. Kamwe sitazisahau." Naye akashikwa, akafungiwa nje, kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu. Alifungiwa nje, bila rehema, naye akaangamia. Na bo—bonge hilo lingali limesimama pale leo. Wanadai (sijui) ungeweza kuvunja kipande chake kimoja na kitakua tena, nguzo ya chumvi. Ukiwahi kuona sinema hiyo ya *Sodoma na Gomora*, utaona ile nguzo asili ya chumvi iliyosimama pale.

88 Sasa, ipo tofauti kati ya nguzo ya chumvi na Nguzo ya Moto. Unaona? Inakubidi kugeuka upande mmoja. Naam.

89 Angalia, katika wakati wa Yohana Mbatizaji. Katika wakati wa Yohana Mbatizaji, walipatikana sita waliokuwa wameshinda. Nyakati zote, wamekuwa na washindi. Katika wakati wa Yohana walikuwa na sita, hao walikuwa ni Yusufu na Mariamu, Zakaria na Elizabeti, Simeoni na Ana. Mwanamume na mwanamke, mwanamume na mwanamke, mwanamume na mwanamke; unaona, mfano wa Kristo, Kanisa; Kristo, Kanisa; Kristo, Kanisa; Kristo, Kanisa. Unaona? Unaona?

90 Angalia, inaanzia kutoka kwa mtu wa kawaida. La, Mu-. . . Yusufu, mtu wa kawaida, Yusufu, alikuwa na kazi gani? Seremala. Halafu kuhani, yeye alikuwa nani, unaona? Mhudumu katika nyumba ya Bwana; Zakaria. Na kutoka kwa huyo, kwa Simoni, nabii na nabii mke. Unaona?. . .?. . . Kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu. Amina. Hivi hamwoni? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Kikamilifu.

Sita walishinda. Hao wengine wote, walitoa dhabihu yao na kila kitu, bali hawa walikuwa Wateule. Walishinda.

91 Angalia kila wakati wa kanisa. Hao hao hushinda wakati hao, kila mwana kutoka katika kila wakati wa kanisa, hushinda jaribio la wakati huo. Nina Maandiko hapa. Sidhani kweli tuna wakati wa kulimalizia, bali tunajua kila mmoja wa nyakati za kanisa. Ni vile vile leo. Ni kama tu mtu fulani ambaye ni . . .

92 Unaona, kama nilivyosema hapo mwanzoni, unazaliwa ukiwa umeshindwa. Na kuzaliwa huko hakuwezi kamwe kukuleta kwenye—kwenye Uzima, kwa kuwa unazaliwa ukiwa umeshindwa. Nawe uko katika ulimwengu ulioshindwa, miongoni mwa watu walioshindwa, miongoni mwa kanuni za imani zilizoshindwa, madhehebu yaliyoshindwa. Inakubidi kufikia ushindi kwa njia fulani.

93 Ni kama tu yungiyungi. Mahali palipo . . . Yungiyungi, nafikiri, ni moja ya maua mazuri sana yaliyopo. Ninapenda sana zile yungiyungi za kala na za kidimbwini. Nafikiri hakuna kitu kinachokaribia uzuri wa yungiyungi kubwa la kidimbwini, liitwalo yungiyungi la majini. Jinsi linavyonawiri! Sasa, linatoka wapi? Ni mbegu ndogo, huko chini ya kidimbwi chenye matope, kichafu sana. Na mbegu hiyo ndogo, hata hivyo, kunawiri kote kutakakopata kunawiri ndani yake, kumo ndani yake wakati uo huo, wakati likiwa kwenye matope hayo. Lakini inabidi lishindane, kila siku, likijua ya kwamba kuna kitu fulani. Ni jeusi. Ni chafu. Lina kinyaa. Linateleza. Katika utelezi huo linamoishi, hata hivyo linajipenyeza kupitia kwenye matope, kinyaa, na maji, na mahali palipotuama, mpaka linatokeza kichwa chake juu, katika nuru, na kuonyesha kile ambacho kilikuwa kimefichwa ndani yake wakati huo wote.

94 Nafikiri huyo ni mshindi, ambaye, wakati mmoja alikuwa katika dhambi, wakati mmoja alifanya mambo yaliyokuwa mabaya, hajali hilo sasa. Wakati mmoja ulifanya mambo mabaya, wakati huo, sasa kwa nini uangalie kwenye hicho kidimbwi tena? Unaona? Angalia, unaninii . . .

95 Mungu, kwa kuchagua Kwake tangu zamani, unaona, ameifufua mbegu hii, nayo inajipenyeza, unaona, ikija kwenye nuru. Na sasa, juu ya hayo yote, imeshinda. Unaona? Haijidhihirishi *kule* chini. Inaamka, ipate kujionyesha.

Wala na wewe pia, katika dhambi za—zako, na uzinzi, na kila kitu ulichoishi ndani yake. Hukuonyesha chochote. Lakini kulikuwa na mbegu mle ndani, nayo ilipata nafasi ya kujipenyeza ikaingia kwenye Nuru. Na sasa uko katika Uwepo wa Yesu Kristo, ukiwa na Nuru ya Mwana. Ilionyesha dhahiri kile ulichokuwa hapo mwanzo. Unaona yale ninayomaanisha? Uliona Nuru. Ukachanua. Ulifungua moyo wako, na sasa wewe ni yungiyungi.

96 Mnakumbuka ujumbe wangu juu ya yungiyungi? Kasisi Yungiyungi, jinsi anavyofanya bidii. “Na, hata hivyo, yeye hasokoti. Hata hivyo, Sulemani, katika fahari yake yote, havikwi kama mojawapo ya haya.” Yeye—yeye—yeye—yeye—yeye. . .Hebu mwangalie. Yuko tayari kuninii. . .Hajichukulii kitu. Yungiyungi hajali chochote juu ya nafsi yake. Anafanya nini? A—anatupa uzuri wake nje, maisha yake, kusudi wengine wapate kuona. Maisha yake yanaonyeshwa wazi, kusudi wengine wapate kuona fahari yake, kile kilicho ndani yake, kilichokuwa ndani yake kwenye yale matope. Sasa yeye yuko juu.

Huyo ni mshindi. Ameshinda matope. Ameshinda mambo ya ulimwengu. Na sasa anajitoa nafsi yake bure. Kila mtu anaweza kumwangalia. Maisha yake, huwezi kuyaelekezea kidole. Unaona? Yeye ni mshindi halisi. Huwezi kusema lolote juu yake sasa. Unasema, “Ametoka kwenye matope.” Bali hayuko kwenye matope sasa. Yuko juu yake. Amina. Huwezi sasa kuelekeza kidole huko nyuma kwa yale aliyokuwa. Yeye ni kitu gani sasa? Yuko juu.

97 Ndipo nyuki anapitia pale na kusema, “Hayo ni manukato mazuri sana. Ninaamini nitaenda na kupata sehemu yangu.”

98 Yeye anafungua tu moyo wake, “Njoo sasa. Vema.” Kila kitu kinachukua kutoka kwake. Unaona? Yeye, yeye ni mchungaji halisi. Anaonyesha Utukufu wa Mungu. Hebu angalia anakotoka. Ilibidi ashinde, apate kufanya hivyo.

99 Wakati mmoja, mwanamume ama mwanamke huyo alikuwa mdogo na mzuri, mrembo. Walikuwa na majaribu mengi ya kuvuka, bali walishinda hayo. Unaona? Walishinda. Sasa wanaonyesha uzuri halisi wa Kristo katika maisha yao. Angalia, kuonyesha, kupitia katika matope.

100 Yesu alitupa mfano, jinsi ya kufanya jambo hilo. Sasa tunataka kujua jinsi ya kushinda. Yesu alitwambia jinsi ya kufanya jambo hilo. Unaona? Unyenyekevu! Alijifunga, akachukua kitambaa, na kuwatawadha wanafunzi miguu na kuipangusa. Mungu Mwenyewe wa Mbinguni alijishusha.

101 Hatutaki kuaibishwa. Hiyo ndiyo sababu wanawake hawataki nywele zao zikue; ndiyo sababu hawataki kuvaa kama vile mabibi wanavyopaswa kuvaa. Kama vile, wanaume hawataki, unaona, ni jambo lile lile. Hawataki. Wao, wanaaibika.

Lakini, Yesu, daima! Angalia kwamba Yeye alikuwa ni Nani. Ukuu! Nitasema jambo fulani. Ukuu hujidhili. Ki*kuu* hujishusha. Ukuu!

102 Nimekuwa na majaliwa ya kupata, kukutana na watu wakuu. Na ni jamaa hawa walio na nguo za kubadilisha, na senti hamsini mfukoni mwao, na kupayuka-payuka, huyo ndiye jamaa anayefikiria yeye ni kitu fulani wakati yeye si kitu. Lakini nilisimama karibu na watu wakuu, ninamaanisha watu wakuu

wenye mikono ya mavazi inayoparuza, sijafu. Wanakufanya ufikiri wewe ndiwe mtu mkuu. Unaona?

Ukuu ni unyenyekevu. Msisahau jambo hilo, Kanisa. Ukuu unadhihirika katika unyenyekevu, si jinsi unavyoweza kuwa safi.

Simaanishi mchafu, sasa. Ni—ninamaanisha mnyenyekevu katika roho. Mnaona? Simaanishi ku—kutoka tu na . . . Kwenda kuoga na kujiweka nadhifu. Hilo, unapaswa kufanya hivyo. Unajua hivyo. Unaona?

Lakini ninazungumza juu ya unyenyekevu, unyenyekevu halisi, si kitu cha kujifanya. Kitu ambacho ni, ambacho ni unyenyekevu halisi.

103 Yesu alitwambia jinsi ya kufanya jambo hilo. Yeye alishinda. Kunamaanisha . . . *Kushinda* kunamaanisha "kustahimili jaribio," hiyo ni kweli, kama vile watakatifu wote wa kale walivyofanya; kama Yesu alivyofanya: miongoni mwa adui Zake wote, Yeye alistahimili jaribio. Kila kitu alichojaribiwa, alikistahimili. Alipokabiliwa na maradhi, Naye akiwa ni Masihi, Yeye aliwaponya. Alipokabiliwa na mauti, aliwafufua. Alipokabiliwa na Kalvari, kifo Chake Mwenyewe, alikishinda kwa kujisalimisha Mwenyewe. Kwa nini? Kwa Neno. Kasema, "Livunjeni Hekalu hili, Nami katika siku tatu nitalisimamisha." Neno lilisema hivyo. Mnaona? Alipokabiliwa na mauti, Yeye aliyashinda. Alishinda mauti. Alipokabiliwa na kuzimu, Yeye alishinda kuzimu na kushinda kuzimu. Naam. Alipokabiliwa na kaburi, Yeye alishinda kaburi. Kwa nini? Yote kwa Neno, na unyenyekevu. Loo, jamani! Huyo hapo Mtu aliye halisi. Huyo hapo unayepaswa kumfanya mfano wako. Mnaona? Alishinda kila kitu, akakishinda.

104 Angalia. Jaribio lilikuwa kwa ajili Yake. Unajua hilo? Biblia ilisema, "Alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi." Alijaribiwa na—na kunywa pombe. Alijaribiwa na wanawake. Alijaribiwa na kila kitu ambacho mtu angejaribiwa. Alijaribiwa na kila kitu tunajaribiwa nacho. Yeye alikuwa ni Mwanadamu, na hata hivyo usingeweza kumtia alama. Naam, bwana.

105 *Kushinda* kunamaanisha "kumtambua ibilisi katika kila moja ya hila zake." Watu wengi husema, "Hakuna ibilisi. Ni wazo tu." Usiamini jambo hilo. Kuna ibilisi halisi. Yeye ni halisi tu kama ulivyo wewe, ama mtu yeyote. Ibilisi halisi, na huna budi kutambua kwamba yeye ni halisi. Inakupasa kujua yeye ni ibilisi. Ndipo, wakati ule ule u—unapomtambua, na kujua ya kwamba yeye ni ibilisi na anakupinga, basi, ili ushinde, lazima utambue ya kwamba Mungu aliye ndani yako ni mkuu na ana nguvu zaidi kuliko yeye, ya kwamba Yeye aliye ndani yako amemshinda tayari. Na, kwa neema Yake, wewe unaweza

kumshinda hata na zaidi. Amina. Huko ndiko kushinda halisi, unapotambua.

106 Unaangalia nyuma, unasema, "Ninafanya jambo *hili* na ninafanya jambo *lile*," basi, la, wewe—wewe, wewe umeshindwa.

"Lakini hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu, wanaoenenda si kwa jinsi ya mwili, bali kwa Roho." Ndipo unatambua ya kwamba umeshinda.

Nawe unajua ya kwamba yeye ni ibilisi. Huwezi kusema, "Nina ugonjwa, nami si—si—si—siamini ni ugonjwa." Loo, naam, ni ugonjwa. Una kansa, wewe "huamini ni kansa." Ni kansa. Ni kansa.

Lakini, kumbuka, "Yeye aliye ndani yako ni mkuu kuliko yeye aliye katika dunia." Huna budi kutambua ya kwamba Roho Mtakatifu aliye ndani yako tayari ameshinda kitu hiki. Naye yumo ndani yako, nawe unaweza kushinda kwa Yeye. Hilo ni la busara kabisa, sawa kabisa na jinsi ambavyo Maandiko yameandikwa. Kushinda!

Sina budi kuharakisha. Tayari nina dakika arobaini na tano sasa. Kweli ninapitisha wakati sasa.

107 Angalia, kushinda! Mungu aliye ndani yako ni mkuu kuliko yeye aliye ndani yake. Mungu wa ulimwengu si mkuu kama Mungu wa Mbinguni, ambaye yuko ndani yako, si zaidi ya vile giza linavyoweza kusimama mbele ya nuru.

108 Sasa, giza haliwezi kusimama mbele ya nuru. Sijali kuna giza jinsi gani, nuru italiondoa. Haliwezi kustahimili. Utukufu! Lakini hebu chukua giza kiasi unachotaka, na ujaribu kusimama dhidi ya nuru wakati mmoja, uone yatakayotukia.

Huyo Ndiye aliye ndani yako, ni Nuru. Na yule aliye katika dunia ni giza. Kwa hiyo, Nuru imethibitisha kushinda giza, na mtu aliye katika Kristo na anajua ya kwamba ameshinda mambo ya dunia. Amina. Haina uhusiano wowote nawe, hata kidogo. Uko huru. "Tukienenda Nuruni, kama Yeye alivyo katika Nuru, na Damu Yake Yesu Kristo yatusafisha na dhambi yote, nasi twashirikiana sisi kwa sisi." Haya basi.

109 "Yeye aliye ndani yako ni mkuu kuliko yeye aliye katika dunia." Sasa, kama ukiangalia nyuma na unahukumiwa, basi ungali uko katika dunia. Lakini kama unaishi juu ya hayo, basi yeye aliye ndani yako amekuongoza ukawa juu ya giza.

Ni kama vile yungiyungi, yeye yuko juu ya giza la matope. Yuko juu ya giza la maji yenye matope. Yuko katika nuru, akiakisi uzuri uliowekwa ndani yake kabla hajatoka kwenye matope. Amina.

110 Sasa na—najisikia kama Mkristo anayepiga mayowe. Kile kilichokuwa mle ndani kwa njia ya Mungu, hapo mwanzo, kimejipenyeza, kikashinda. Kilishinda lile ganda. Kilishinda

matope. Kilishinda maji. Kilishinda kila kitu, na kilikuwa mshindi, na kikaakisi uzuri na Utukufu wa Mungu.

111 Hivyo ndivyo kila mwaminio anavyofanya. Hivyo ndivyo Nuhu alivyofanya. Hivyo ndivyo Lutu alivyofanya. Hivyo ndivyo ilivyo. Angalia jinsi alivyokuwa amechafuka. Hivyo ndivyo Musa alivyofanya. Hivyo ndivyo Yoshua alivyofanya. Hivyo ndivyo Danieli alivyofanya. Hivyo ndivyo Shadraka, Meshaki walivyofanya. Hivyo ndivyo Yohana Mbatizaji alivyofanya; Zakaria, Elisabeti. Hivyo ndivyo ambavyo Simeoni, hivyo ndivyo ambavyo Ana, kila mmoja wao alivyofanya. Walishinda matope yaliyowazunguka na waliyopakwa. Wakapenyeza kichwa chao juu ya kitu hicho, na wakaangaza Utukufu wa Mungu. Hivyo ndivyo Mkristo halisi anavyofanya.

112 Kumbukeni, Yesu alimwonyesha jinsi jambo hilo linavyofanywa. Siku arobaini za jaribio. Alijaribiwa zaidi ya mtu yeyote angaliweza kujaribiwa, katika kujaribiwa kwa Yesu Kristo. Angalia. Yeye alituonyesha jinsi jambo hilo linavyofanywa.

Sasa nitafunga, katika dakika chache tu.

113 Angalia. Alituonyesha jinsi inavyofanywa. Yeye alilifanya namna gani? Kwa Neno. Hivyo ndivyo alivyolifanya, kwa kuwa Yeye alikuwa Neno. Naye Yesu alisema, "Mkikaa ndani Yangu, na Maneno Yangu yakae ndani yanu," mmerudi kwenye Neno tena, Neno la ahadi. Neno la ahadi ni nini kwa kila Mkristo? "Yeye aliye ndani yenu ni mkuu kuliko yeye aliye katika dunia." Basi ninashindaje? Si mimi, bali ni Neno lililo ndani yangu. Hilo Neno ni Mungu. Ndipo ninashinda mambo ya dunia, kwa sababu ni Neno lililo ndani yangu. "Mkikaa ndani Yangu, Maneno Yangu ndani yenu, basi ombeni tu mtakalo." Endelea tu kupenya juu. Unakuja kwenye kilele, hakika kabisa. Unaona? Huna budi kuja kwenye kilele.

114 Siku Zake arobaini za kujaribiwa, kwa Neno la Mungu Yeye alishinda. Ninataka kuelezea jambo fulani hapa kwa dakika chache tu. Shetani alifanya mashambulizi matatu makubwa juu Yake katika kujaribiwa kule. Angalia. Daima huwa katika hayo matatu. Msisahau jambo hilo. Unaona? Yeye alifanya mashambulizi matatu makubwa, kutoka yale makubwa sana hata madogo kabisa. Alijaribu alivyoweza kumshinda Yeye. Lakini Yeye alikuwa ni Neno. Amina. Alitumia nini? Yeye Mwenyewe, Neno. Mashambulizi matatu makubwa ama hujuma za Shetani juu Yake, bali Yeye alikabiliana nalo kwa Neno. Kila shambulizi, Yeye angeweza kulistahimili kwa Neno. Angalia jambo hili sasa, kutoka lililo kubwa sana hata lililo dogo kabisa.

115 La kwanza aliloshambulia, lilikuwa ni kutumia nguvu Zake kuu. Ambapo, Yeye alijua alikuwa ni Neno. Alijua mahali Pake. Mnaamini alipajua? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] "Mimi Mwana wa Adamu." Alijua mahali Pake. Naye

Shetani akaja na kumtaka atumie nguvu Zake Mwenyewe kwa nafsi Yake, kujilisha, anataka ajilishe Mwenyewe. Alikuwa na njaa. Mtu akipata njaa, anaweza kufanya karibu jambo lolote. Ataiba, atanyang'anya, ataomba, atakopa, chochote kile. Unaona? Alikuwa na njaa hiyo ya chakula. Na Shetani akatumia shambulizi lake la kwanza kubwa juu Yake, kuchukua nguvu Zake alizokuwa amepewa za kushindia na kuzitumia kwa nafsi Yake. Hakuzitumia kwa nafsi Yake. La. Alizitumia kwa wengine. Hiyo ni kweli. Alizitumia kwa wengine, si Yeye Mwenyewe. Hazikuwa kwa ajili Yake. Ingawaje, angaliweza kufanya hivyo. Hakika angaliweza kufanya hivyo.

116 Lakini mnaona jinsi ibilisi anavyojifanya? Ibilisi anakutaka umjali. Yeye alijali yale tu Baba aliyosema afanye. Hiyo ni kweli.

Alisema, "Mbona," Shetani akasema, "imeandikwa, 'Atawaagiza Malaika . . .'"

117 Yeye akasema, "Naam, lakini pia imeandikwa . . ." Unaona? Haya basi. Unaona? Yeye alijua kwamba alikuwa ni Nani. Shetani alininii . . .

Wazo linaingia ndani zaidi ya vile lilivyoandikwa. Unaona? Ni uvuvio. Kiini kiko ndani Yake, unaona, jinsi vile lilivyo hasa.

118 Ingawa angaliweza kufanya hivyo, Yeye hakufanya hivyo. Bali kamwe ha—hakusikiliza ushauri wa Shetani.

Sasa, hili hapa jambo zuri. Unaona? Wakati mwingine Shetani anaweza kukuchukua, na wakati unapowazia ya kwamba unafanya mapenzi ya Mungu, na anaweza kukupa ushauri, utaangukia hilo. Naam, bwana. Kweli anaweza.

119 Sasa hebu na tuchukue tu, kwa mfano, kama vile dada zetu. Wao ni warembo. Naye anaweza kukufikisha mahali fulani, ambapo, unaachilia nywele zako zikue, hukutambua. Zilionekana nzuri sana ukiwa nazo, na, muda si muda wajua, kwa namna fulani unashikwa na kiburi, kidogo juu ya wengine. Baadhi yenu wanaume, mnajua ninalomaanisha. Unaona? Naye anaweza kuchukua jambo lilo hilo na kukupa ushauri kwake. Hiyo ni kweli. Inakubidi kushinda jambo hilo.

Kumbuka tu, unamwishia Mungu. Una kusudi moja, na hilo ni Yesu Kristo. Nje ya hilo, hakuna jambo lingine linalojalisha. Huyo ni Yeye. Halafu, pili, kwa ajili ya familia yako. Halafu, tatu, kwa ajili yako mwenyewe. Lakini, kwanza, kwa ajili ya Mungu; pili, kwa ajili ya familia yako; na halafu, kwa ajili yako wewe. Wewe ni namba tatu; huo ndio mwisho wa safari. Jiweke wa mwisho; Yeye alifanya hivyo.

120 Angalia yale angalifanya. Kasema, "Ningeweza kumwita Baba Yangu, nizungumze Naye, Yeye mara moja angeniletea majeshi kumi na mawili ya Malaika." Wakati, mmoja wao angeweza kuuangamiza ulimwengu. Kasema, "Kama Ufalme Wangu ulikuwa ni ulimwengu huu, basi raia Wangu

wangepigana. Lakini Ufalme Wangu ni wa huko Juu." Haya basi. Unaona? Angaliweza kufanya hivyo, bali hakufanya. Unaona? Ingawa, Yeye angaliweza kufanya jambo hilo. Kamwe hakusikiliza ushauri wa Shetani.

121 Sasa, je! umewasikia watu wakisema, "Kama—kama unaamini kuna—kuna mponyaji wa Kiungu...Kama wewe ni mponyaji wa Kiungu...Nenda kamlete mponyaji wako wa Kiungu. Nina mtu hapa, mgonjwa. Ningetaka kumwona akimponya." Unaona ibilisi yule yule? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Yeye anajaribu kukupa ushauri. Anajaribu kukufanya umsikilize badala ya Mungu. Lakini mtumishi halisi, wa kweli wa Mungu atasikiliza na kuona yale Baba asemayo, kwanza. Unaona?

122 Ni kama yule mtoto mchanga wa Stadsklev, walipotuma habari hapa. Na Bibi Stadsklev akasema, "Ndugu Branham, nilikupigia simu kutoka Ujerumani." Kulikuwako na jeshi la Marekani, likiwa na moja ya ndege zao za jeti imewekwa hapa nje uwanjani, ingenirusha kwenda Ujerumani na kunirudisha, katika siku moja. Yeye alikuwa ni kasisi wa jeshi. Na mtoto huyo mchanga alikuwa amelala, amekufa. Na maskini mama huyo akipiga mayowe, akasema, "Sikilizeni!" Kasema, "Ninajua. Nilisimama pale pale na kumwona mwanamke huyo ameshika huyo mtoto mchanga aliyekufa mikononi mwake, aliyekufa asubuhi hiyo. Nilimwona Ndugu Branham akitoka moja kwa moja pale nje, akaweka mikono juu ya mtoto huyo aliyekufa, naye akafufuka." Kasema, "Huyu ni mtoto wangu mchanga, Ndugu Branham." Hakujapata kuwa na kifo katika familia yao. Unaona? Na maskini kitoto hiki kidogo kilishikwa na ugonjwa asubuhi moja na kikafa alasiri hiyo.

Hawa hapa hao wote wamesimama kumzunguka, na wakitoa unabii na kadhalika, "Mtoto huyu mchanga atafufuka," na mambo yote namna hiyo.

123 Nikasema, "Vema, hilo ni zuri mno, Dada Stadsklev. Lakini hebu nione yale Baba anayosema."

Nilitoka nikaenda mwituni. Nami nikaomba. Nikarudi ndani; alikuwa tayari amepiga simu mara mbili ama tatu kabla sijarudi kesho yake asubuhi. Hakuna kitu.

Daktari akasema, "Vema." Kasema, "Kama hivyo ndivyo ilivyo, kama una imani kama hiyo, mama, kamwe hatutaruhusu mtoto aondolewe hospitalini. Acha akae papa hapa. Wewe kaa papa hapa naye. Hilo ni sawa."

Ndugu Stadsklev alienda akamwona meja wa jeshi. Wakasema, "Hakika. Tutamsafirisha kwa ndege aje huku, na kumrudisha."

124 Na kulikuwako na ndege iliyowekwa pale, ikingojea, kunipeleka huko asubuhi hiyo na kunirudisha usiku huo, huko Ujerumani, kwenda Heidelberg, Ujerumani, kwa ajili ya

kufufuliwa kwa mtoto huyu mchanga. Nikasema, "Hakika, Mungu anaweza kumfufua, bali hebu na tuone mapenzi Yake ni nini."

125 Ndipo nikatoka, nikaomba usiku kucha. Hakuna jambo lililotukia. Nikarudi kesho yake asubuhi; hakuna jambo lililotukia. Ndipo nikaanza kuingia chumbani. Papo hapo nikaangalia pale, na pale ilisimama ile Nuru imening'inia pale mlangoni. Kasema, "Usiweke mkono wako juu ya hilo. Usikemee jambo hilo. Huo ni mkono wa Mungu."

126 Nikampata kwenye simu. Nikasema, "Dada Stadsklev, mzike mtoto wako mchanga. Ni mkono wa Bwana. Ni mapenzi ya Mungu. Jambo fulani lingempata mtoto huyo mchanga maishani. Wewe mwache aende mahali ambapo Mungu anajua alipo. Unaweza kwenda kwake sasa. Akiishi, hutaweza. Mwache tu jinsi hiyo."

127 Yule mhubiri mashuhuri wa Kilutheri huko Ujerumani aliandika barua na kusema, "Jinsi ninavyoweza kuthamini, yale, Ndugu Branham kungojea apate uamuzi huo dhahiri kutoka kwa Mungu, kabla hajasema jambo lolote."

Jambo ndilo hilo. Shikilia uamuzi wa Mungu. Haidhuru wengine wanasema nini, ama chochote kile, usishauriane na Shetani, hata kidogo.

128 Kama Shetani akisema, "Sasa, ubatizo wa maji, jina la 'Baba, Mwana . . .'" Kama hilo, hata akitoa ushauri, wewe achana nao. Mungu alisema vinginevyo. Akisema, "Wewe ni mtu mzuri, haikubidi kuwa . . . Wewe ni mwanamke mzuri, haikubidi kufanya . . ." Usishauriane. Kama Neno linasema vinginevyo, wewe dumu na Neno haidhuru ni kitu gani. Huo ndio mfano ambao Yesu alikupa, na hilo hapo shambulizi kuu, unaona, alilomshambulia nalo.

129 Halafu, shambulizi la pili. Nitaharakisha. Inaonekana tu kana kwamba wakati unakwenda mbio sana. Shambulizi lingine kuu lilikuwa, ambalo alimshambulia nalo, lilikuwa kwamba yeye angekuwa mwenye majigambo.

Na jinsi ambavyo hilo kweli huwapiga watumishi wa Mungu, kujivuna, kuonyesha yale unayoweza kufanya. "Utukufu kwa Mungu! Haleluya! Mimi ni mkombozi! Mimi ni *ninii*." Unaona? Unaona?

130 "Njoo huku juu, juu ya hekalu, na uketi hapa chini." Alimjaribu kufanya jambo hilo. Sasa, kumbukeni, Yeye alijaribiwa kufanya jambo hilo, sana. Kasema, "Sasa, kama unataka kuwa kitu fulani mbele za watu, simama hapa juu ya hekalu hili, uruke." Unaona? "Nitakupa Andiko kwa ajili yake, kwa maana imeandikwa, 'Atakuagizia Malaika, usije, wakati wowote, ukajikwaa mguu katika jiwe. Atakuchukua.'" Kumfanya mtu mwenye maringo, kuonyesha mamlaka Yake.

131 Hakuna mtumishi wa kweli wa Mungu anayefanya jambo hilo. Ukimwona mtu akijionyesha, kifua mbele, na kila kitu namna hiyo, kumbuka tu, kuna kasoro pale. La. Mungu hataki jambo hilo. Yesu aliweka mfano. Angaliweza kufanya jambo hilo. Hakika angaliweza kulifanya, bali hakulifanya. Hakuna mtumishi wa Mungu anayejigamba, kwa nafsi yake, kujaribu kuchukua nguvu za Mungu na kujionyesha juu ya mtu mwingine.

132 Mnakumbuka Musa alifanya jambo hilo? Mnakumbuka? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mungu alimpa nguvu kufanya lolote alilotaka kufanya; akamfanya nabii. Alishuka akauendea ule Mwamba, naye akaupiga huo Mwamba mara ya pili. Hilo lilikuwa ni kinyume cha mapenzi ya Mungu.

Mungu alisema, "Sema na ule Mwamba. Usiupige tena. Utavunja mifano yo—yo—yote hapa. Mwamba utapigwa tu mara moja." Lakini yeye alinena juu ya unyonge wa Neno wakati alipofanya jambo hilo; Hilo halikutosha. Naam. Neno ndilo lililokuwa likiendelea. Huo Mwamba ulikuwa ni Neno. Unaona?

133 Yeye, mara ya kwanza, aliupiga Mwamba na maji yakatoka. Ndipo wakaona kiu tena. Yeye akasema, "Sasa rudi ukaseme na ule Mwamba." Ulipigwa mara moja tu. Unaona?

"Kule kutotosheleza kwa Neno." Musa alishuhudia hilo. "Neno halikuwa kweli; Yeye alipaswa kupigwa tena."

134 Kwa hiyo Musa alishuka akaenda kule na kuupiga ule Mwamba namna hiyo, akasema, "Toka!" Hayakutoka, kwa hiyo akaupiga tena, na kusema, "Toka! Ninakuamuru utoke." Ndipo maji yakatoka.

135 Mungu akasema, "Njoo huku juu. Njoo huku. Ulijitukuza mwenyewe. Ulichukua nguvu Zangu; badala ya kunitakasa Mimi, ulijitakasa mwenyewe. Sasa hutaenda kwenye ile nchi. Angalia kule, angalia jinsi ilivyoonekana; lakini, hapa, utaondoka papa hapa." Loo, jamani! Hakujapata kuwa na mtu kama Musa, mwajua. La, la.

136 Wakati alipokuja kwenye lile onyesho na Yesu, alisema, "Panda huku hekaluni kisha uruke."

137 Akasema, "Imeandikwa," amina, "'Usimjaribu Bwana Mungu wako.'" Unaona? Yeye alikabiliana naye kwa Neno, katika hilo, na kila shambulizi kubwa.

138 Hakuna mtumishi wa kweli anayejaribu kujigamba, kwa—kwa nguvu za Mungu. Akifanya hivyo, anashindwa papo hapo.

139 Shambulizi la tatu kubwa, Shetani alijitolea kumwachia ufalme huu. Alifanya hivyo. Shetani alisema, "Unaona falme hizi za ulimwengu? Hizi ni zangu. Ninafanya nazo lolote nipendalo. Nitakuachia."

Lakini, kumbuka, alikuwa akijaribu kumfanya aziache bila msalaba. Kama angalifanya hivyo, tungepotea. Yeye angeweza

kuuchukua huo ufalme. Lakini hana budi kufuata ninii . . . Hana budi kurudi. Alijaribiwa kufanya hivyo, sasa. Kifo ni jambo gumu. Alijaribiwa kuchukua uhuru Wake na kuwa Mfalme wa ulimwengu, bila ya msalaba. Lakini, kama angalifanya hivyo, raia Wake wangelikufa. Shetani angalifurahia kufanya mapatano hayo Naye. Lakini Yeye alisema, "Rudi nyuma Yangu, Shetani." Hakufanya hivyo.

140 Yeye alikuja na akateseka, na akachukua njia iliyo ngumu, inayoparuza. Alichukua njia ya mateso. Alichukua njia ya mauti.

Je! sisi, asubuhi ya leo, tuko tayari kufanya, kupitia njia ile ile aliyopitia? Je! tuko tayari kufa? Tuko tayari kujitoa kwa Mungu, kuachana na ulimwengu wote na kadhalika, kumtumikia? Unaona?

141 Sasa, Yeye alishindwa kufanya hivyo. Shetani, kwa hiari yake, alitaka ku—kumwachia Yeye. Lakini Yeye hakufanya hivyo. Ingawa Yesu alijaribiwa, Yeye alishinda kwa ajili yetu. A—alivumilia majaribu yote kwa ajili yangu na kwa ajili yako. Unaona? Angaliweza kuuchukua wakati uo huo. Lakini kwa nini akapitia njia hiyo nyingine? Kusudi tuweze kuja, kuwa pamoja Naye. Na kama Yeye alilipa gharama kama hiyo, basi sisi tungekuwa duni jinsi gani kutoipitia? Wakati, kumbuka, hakuna kitu hapa, hata hivyo.

142 Kama ukiishi miaka mia moja, utakuwa nini? Wazimu, na akili zako zimepotea, umekuwa mlemavu kabisa, na mzee na mtu anayetetemeka. Huko ndiko unakoelekea, na huo ndio mwisho wake. Njoo sasa, shinda jambo hilo. Unafanyaje jambo hilo? Kwa Neno. Yale Neno lisemayo, unayafanya. Tembea kwa unyenyekevu. Ishi mbele za Yesu.

143 Yeye alivumilia mambo yote kwa ajili yako na yangu. Yeye ndiye mfano wetu jinsi ya kushinda kizazi chetu kiovu, kama Yeye alivyokishinda kizazi Chake kiovu.

144 Kumbuka, wakati alipokuja duniani, kuna kutokuamini kwingi vile vile, ama zaidi, kuliko kunavyokuwa wakati wowote. Hakukumsumbua hata kidogo. Walipomwita ibilisi badala ya Mungu, wakati walipomwita kila kitu ambacho kingaliweza kufanywa, halikumsumbua hata kidogo. Yeye alikuwa na kusudi moja, "Kumjali Baba. Kulitii Neno." Neno ni Mungu. Yeye alikuwa na nia moja.

145 Wakati mwingine tunajaribiwa kurudi nyuma. Wengi wenu, mnajaribiwa kurudi nyuma kwenye dhehebu, kurudi nyuma na kuchukua, maana ulimwengu mzima unasema, "Wewe ni wa dhehebu gani? Unashiriki kwenye kanisa gani?" Tunajaribiwa kufanya hivyo; sisi sote tunajaribiwa. Dada zetu wanajaribiwa kurudi nyuma, kurudi nyuma na kujiunga na hayo makanisa mengine, pamoja na baadhi ya Assemblies, ama makanisa ya Mungu, ama baadhi yao; wangali ni Wapentekoste, wanawaacha

mkate nywele zenu, na kuvalia kwa karibu kila namna mnayotaka. Unaona? Unajaribiwa kufanya hivyo, kurudi nyuma na kuwa mtu anayependwa na kizazi hiki kiovu tunachoishi pamoja nacho.

Wakati, hii ndiyo dhambi iliyo kubwa sana ya siku zetu. Ndiyo dhambi iliyo kubwa mno miongoni mwa watu wetu, kupenda anasa za ulimwengu, kama vile Biblia ilivyosema Laodi-. . . Wakati wa Laodikia ulivyokuwa. Ni wa kilimwengu, "Tajiri, hauna haja na kitu; haujui kwamba uko uchi; wenye mashaka, mnyonge, na kipofu." Hiyo ndiyo dhambi ya siku yetu. Wakati unaposikia Neno la Mungu likiikaripia, ndipo unapopitia njia nyingine, hupendwi na ulimwengu. Unajaribiwa kurudi.

146 Ninajua. Unaendelea kuniambia. Ninajua unasema, "Wakati wote." Ninajua unachoshwa na mimi nikirudiarudia mambo haya. Ninachoshwa na kukuona ukifanya hivyo, pia, hiyo ni kweli, dhambi hii ninayojaribu kukwambia habari zake. Unasema, "Unayarudiarudia ya nini?" Acha kufanya hivyo, basi. Ninajaribu kuyaokoa maisha yako, kwa Neno. Ninachoka, pia. Kwa hiyo, nyoosha tu mambo. Hii ni dhambi, haipaswi kufanywa. Naam, bwana.

147 Tunapaswa kushinda mambo haya. Tunatarajia kujaribiwa nayo, dunia. "Mtu ukiipenda dunia, mambo yaliyomo katika dunia, kumpenda Mungu hakumo ndani yako," Yesu alisema.

148 Sasa tutafunga tu, na kusema hivi. Kuna tuzo kwa ajili ya mshindi.

149 Hebu niwasomee jambo fulani hapa. Fungueni katika Biblia zenu. Hebu turudi katika Ufunuo, wa 3, mlango wa 2. Angalieni hapa sasa, mambo haya yote ambayo nimekuwa nikiyazungumzia, kushinda. Sasa hebu jiangalie tu wewe mwenyewe na uone. Jichunguze mwenyewe katika kioo cha kiroho cha kujiangalia, uone kama wewe umeshinda.

150 Sasa, ujumbe wa kwanza, kwa ma—malaika wa Efeso, ninawatakeni msikilize yale Yeye aliyosema. Na Ufunuo, mlango wa 2, kifungu cha 7. Hili ni kwa wakati huo wa kanisa, wakati alipowaambia yote yale waliyofanya, "Kuacha upendo wao wa kwanza." Kifungu cha 7:

> *Yeye aliye na sikio, na alisikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa. Yeye* (mtu, si kanisa) . . . *Yeye ashindaye—ashindaye,* nitampa *kula matunda ya mti wa uzima, ulio katika bustani ya Mungu.*

Unaona? Washindi katika Efeso.

151 Sasa, wa pili ulikuwa ni Smirna. Sasa, kwa washindi katika huo, tusikilize hili. Sasa, kifungu cha 11.

> Hebu *yeye—yeye* aliye *na sikio, na alisikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa. Yeye ashindaye hatapatikana na madhara ya mauti ya pili.*

Unaona? Waliishinda.

152 Sasa, hilo, sasa angalia kwenye Pergamo, tutaona kile mshindi alikuwa amemwachia, katika huu. Tutasoma kifungu cha 17, kwa kanisa la Pergamo.

> *Yeye aliye na sikio, . . .*

Huyo, huyo ni mtu binafsi, si kundi lote. Mtu binafsi, huyo ni Bibi-arusi anayetoka, unaona, lile Kanisa.

> Yeye aliye na sikio*, na alisikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa. Yeye ashindaye* nitampa *baadhi ya ile mana iliyofichwa, nami nitampa jiwe jeupe, na juu ya jiwe hilo limeandikwa jina jipya asilojua mtu ila yeye* alipokeaye.

Huyo ni huyo mshindi, wa wakati huo wa kanisa.

153 Sasa, unaofuata ni Thiatira. Hebu tuone mshindi alipata nini katika siku hiyo. Hebu tuchukue kifungu cha 26.

> *Na yeye ashindaye, na kuyatunza matendo yangu hata mwisho, nitampa mamlaka juu ya mataifa,* (Hiyo ni kweli.)
>
> *Na . . . atawachunga kwa fimbo ya chuma,* na *kama* vyombo *vya mfinyanzi vipondwavyo, kama mimi nami nilivyopokea kwa Baba yangu.*

Unaona, "Pamoja Naye, katika kiti Chake cha enzi." Kristo atayatawala mataifa, kwa fimbo ya chuma. Na hili hapa Kanisa linaloshinda, "Limeketi mle ndani, pamoja Naye, kuyavunja mataifa kwa fimbo ya chuma."

154 Sasa hebu tuwapeleke kwenye kanisa la Sardi. Sasa kifungu cha 5 cha mlango wa 3.

> *Yeye ashindaye atavikwa hivyo mavazi meupe, wala sitalifuta kamwe jina lake katika kitabu cha uzima, nami nitalikiri jina lake mbele za Baba yangu, na mbele ya malaika zake* watakatifu.

Hiyo ni kwa mshindi katika Sardi.

155 Sasa, hebu na tuchukue sasa kifungu cha 12. Sasa, hili ni kwa kanisa la—la Filadelfia, katika kifungu cha 12.

> *Yeye ashindaye, nitamfanya kuwa nguzo katika helaku la Mungu wangu, wala hatatoka humo tena kabisa, nami nitaandika juu yake* jina langu*, jina la Mungu wangu, na jina la mji wa Mungu wangu,* huo *Yerusalemu mpya, ushukao kutoka mbinguni kwa . . . Mungu na jina langu mwenyewe, lile jipya.*

156 Angalia kile mshindi alichoahidiwa. Unaona?

Sasa, sasa Laodikia, huo ni wakati wa mwisho wa kanisa. Kutakuwako na washindi fulani mle ndani. Angalia hapa. Wao, kumbuka, kila wakati wa kanisa, lile linalofuata linarithi yote ambayo hizo nyingine zilipewa. Angalia hapa juu. Sasa, hapa, ni baada ya wao kupokea mamlaka haya yote, majina haya mapya, na kila kitu kilichoandikwa, alichoahidi, na kula mana iliyofichwa, na kote kote. Angalia wakati huu wa mwisho wa kanisa, Ufunuo 3:21.

> *Yeye ashindaye, nitampa kuketi pamoja nami katika kiti changu cha enzi,* (amina) *kama mimi* nilivvyoshinda *nikaketi pamoja na Baba yangu katika kiti chake cha enzi.*

> *Yeye aliye na sikio, na alisikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa.*

157 Kuna tuzo kwa washindi. Jipenyeze, ewe yungiyungi. Kama liko ndani yako, weka kando matope na chochote kile, na ujipenyeze ukielekea juu. Naam, bwana. "Kuketi pamoja Nami katika kiti Changu cha enzi."

158 Unajua, wakati mmoja, mama wa Yakobo na Yohana... Hatutapata wakati wa kulisoma. Mama wa Yakobo na Yohana alikuja na kuomba mahali hapa. Unajua hilo? Unakumbuka jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] "Bwana, jalia mwanangu aketi upande mmoja, na mwanangu mwingine upande huo mwingine." Hiyo hapo shauku ya mama kwa ajili ya mwanawe.

Lakini angalia. Lakini, "Mahali hapo," Yesu alisema, "palichaguliwa tangu zamani." Mahali hapo hapakuwapo wakati huo. Kwa nini? Angalia. "Patapewa wale waliokusudiwa." Ati nini? Yule atakayeketi mkono wa kulia, na yule aliye karibu zaidi Naye, walikuwa bado kuwa mshindi. Unaona? Ilikuwa bado... Yeye alisema, "Mi—mimi sitoi jambo hili. Siwezi kutoa hili, bali litatolewa baada ya majaribio kuja." Amina. Unaona? "Siwezi kutoa hili. Lakini baada ya majaribio kuja, wao wataketi mkono wa kulia na mkono wa kushoto. Kuna uzao uliokusudiwa unaongojea jambo hilo huko ng'ambo. Litatolewa kwa wale walioahidiwa hilo. Litatolewa huko, bali jaribio halijakuja bado; hilo, Yeye hajashinda bado." Unaona?

159 Mtu aliyekuwa achukue mahali hapa upande mmoja, na mwingine achukue upande mwingine, karibu na Yeye katika ule Ufalme, halikuwa limetolewa bado, mnaona, huyo hakuwa ameshinda. Jaribio halikuwa limeshuka bado. "Litashuka katika siku za usoni."

"Tukiteswa kwa ajili ya Kristo na Neno Lake, tutatawala pamoja Naye, kwa kuwa Yeye ni Neno." Kumbukeni, "Tukiteswa kwa ajili Yake na Neno Lake, tutatawala pamoja Naye, katika Neno Lake."

160 Angalia. Yeye, Mfano wetu, alishinda, na kisha akapaa juu, baada ya kushinda mauti, kuzimu, magonjwa, kaburi. Kila kitu, Yeye alishinda. "Kisha akapaa juu, na akateka mateka, akawapa wanadamu vipawa." Hilo lilikuwa ni Agano la Kale, pamoja na watakatifu wa Agano la Kale waliokuwa wameshinda. Walimtazamia Mtu kama huyo, nao wakafa kabla Yeye hajafika. Lakini wakati Mtu huyu alipokuja, "Haikuwatangulia wale waliolala mauti." Amina. Huwezi kushindwa, kwa njia yoyote. Uishi ama ufe, inaleta tofauti gani? "Hawatawatangulia." Unaona? Walitazamia jambo hilo.

161 Hata Ayubu kule nyuma, alilitazamia jambo hilo. Yeye alisema, "Ninajua Mkombozi wangu yu hai, na katika siku za mwisho atasimama juu ya nchi." Huyo hapo alikuwa mtu mwenye haki, mtu mkamilifu. Alitoa dhabihu. Alifanya kila kitu ambacho Mungu alimwambia afanye. Alikifanya kwa uchaji na heshima. Alikuwa nabii. Na ndipo Shetani akamjia, apate kumjaribu. (Kama tu vile anavyokuja kukujaribu.) Yeye alifanya nini? Aliendelea kusimama pale.

Mke wake hata alitokea, kasema, "Mbona usimkufuru Mungu ukafe kifo? Unaonekana mwenye majonzi sana ukiketi hapo."

162 Akasema, "Wewe wanena kama mwanamke mpumbavu." Sasa, kamwe hakusema alikuwa mpumbavu, bali alinena kama mpumbavu. Unaona? Kasema, "Wewe wanena kama mwanamke mpumbavu." Kasema, "Bwana alitoa, na Bwana ametwaa; Jina la Bwana na libarikiwe." Alishinda.

163 Alishinda yale majirani waliyosema. Alishinda yale wafuasi wote wa kanisa, Bildadi na wote hao, waliyosema. Alimshinda askofu na yale aliyosema. Alimshinda kadinali na yale aliyosema. Alishinda dhehebu, yale waliyosema. Naye akadumu na kuhesabiwa haki kwa Neno. Amina. Hata hivyo, ilimgharimu kila kitu alichokuwa nacho, hata watoto wake. Alijikuna majipu kwa kigae, akiketi kwenye hili, na hata hivyo alishinda. Na hatimaye wakati ile saa kuu ya majabu ilipofaulu, ndipo mawingu yakafingirika kurudi nyuma.

164 Yeye aliangalia kila kitu cha kweli. Akasema, "Kuna tumaini katika mti kama ukifa; unaishi tena. Na mbegu inaanguka ardhini, inaoza; inaishi tena. Lakini mwanadamu hufa na kutoa roho yake; anafariki dunia. Ndipo watoto wake wanakuja, wanawe, kumheshimu na kumwombolezea; yeye hajui. Hainuki tena. Loo, huyo hapo. Kuna nini? Mimi ni mbegu, pia. Mimi ni kitu fulani, ambacho ni mbegu, nami nitaingia ardhini. Siwezi kuamka tena. Nitalala pale. Loo, nifiche kaburini, niweke katika mahali pa siri hata ghadhabu Yako itakapopita. Niandikie muda na kunihukumu. Kama mawe yanavyolika, maji yanavyolikwangua jiwe." Loo, aliendelea, akisema mambo haya

yote. Angeweza kuona mifano yote huko nje, jinsi ilivyokuwa. Loo, asingeweza tu kuliona.

165 Na, Dada Rodgers, kumbuka wakati nilipohubiri jambo hilo kwenye mazishi ya Busty. Unaona?

166 Jinsi, ambavyo, "Angeliparura jiwe," jinsi ambavyo mambo haya. "Loo, Wewe, nifiche kaburini, na uniweke mahali pa siri." Aliendelea kujipenyeza. Akasema, "Laiti ningalijua. Laiti ningalijua mahali ningeweza kwenda, kwa Mtu ambaye angeweza kuniwekea mikono Yake, mtu mwenye dhambi, na Mungu mtakatifu, na anene Naye kwa ajili yangu." Loo, jamani! "Yuko. Ninajua Yeye Yuko Mahali. Yuko Mtu Pale anayeweza kufanya jambo hilo. Kuna Mtu fulani mahali fulani. Ninaweza kumpata Mtu huyo wapi? Ninaweza kumpata wapi? Nitabisha mlango wake na kuzungumza na Yeye. Laiti Mtu fulani angaliweza tu kuweka mkono Wake juu yangu, na juu ya Mungu, na—na kuniunganishia njia, kuzungumza! Laiti ningaliweza kumpata Mtu huyo! Loo, Yeye yuko wapi?"

167 Alitafuta katika kanisa lake. Alikuwa ametafuta katika madhehebu yake. Asingeweza kumpata Mtu kama huyo.

168 Ndipo kwa ghafla, mawingu yalifingirika yakarudi nyuma, ndipo akamwona Mtu huyo akija. Loo! Moyo wake mzee ulidundadunda kwa furaha. Ndipo jambo fulani likatukia. "Ninajua Mteteaji wangu yu hai. Kuna Mtu kama huyo." Amina. Kungali kuna Mtu kama huyo. "Ninajua Mteteaji wangu yu hai. Na hata ingawa, baada ya mabuu ya ngozini kuuharibu mwili huu, hata hivyo katika mwili wangu nitamwona Mungu, Ambaye nitamwona mimi kwa nafsi yangu. Atasimama juu ya nchi katika siku ya mwisho."

169 Kwenye asubuhi hiyo ya Pasaka, wakati Yeye alipofufuka huko ng'ambo, na mwili wa Ayubu si zaidi ya kijiko kimoja cha majivu, yeye alikuwa akingojea. Yeye alikuwa ni lile Kundi lililoteuliwa. Alifufuka kutoka kaburini na akaingia mjini, pamoja na Ibrahimu, Isaka, Yakobo, Ayubu. Loo, jamani! Amina. Kwa kuwa, walimtazamia Mtu kama huyo.

170 "Na kwa wale Ambao wanamtazamia Kristo kwa mara ya pili," wanaoweza kushinda mambo ya ulimwengu huu, kwa neema Yake, kuingia katika Yeye, na kufunga macho yenu kwa kitu kingine chochote ila Yeye na Neno Lake, "Yeye atatokea mara ya pili katika Utukufu."

"Kwa maana parapanda ya Mungu italia, waliolala katika Kristo watafufuka, hao walio hai na waliosalia watabadilishwa, katika dakika moja, kufumba na kufumbua jicho, watanyakuliwa pamoja, kumlaki Yeye hewani."

171 Kama mimi ni kijiko kimoja cha majivu, ama kama ninaishi wakati atakapokuja, haileti tofauti yoyote kwangu. Amina. Haijalishi, kwa maana nimepata ono. Pazia lilifingirika likarudi nyuma, nami ninamwona. Mtu ambaye angeweza kusimama,

na kuweka mkono Wake juu yangu, mtu mwenye dhambi, na juu ya Mungu mtakatifu. Naye ndiye upatanisho wangu. Yeye ndiye Neno ninaloshindania. "Hapo mwanzo kulikuwako Neno." Yeye ndiye lile Neno, Naye ananiwakilisha, Kule. Amina. Nami nitasema hili kwa sauti kuu, mradi ningali na pumzi, "Yeye ni Ufufuo wangu na Uzima wangu." Na sehemu zingine zote ni mchanga udidimiao. Sehemu zingine zote ni mchanga udidimiao.

172 Kama vile alivyonyakua wale waliotazamia jambo hilo, vivyo hivyo Yeye atamjia kila mtakatifu wa Agano Jipya ambaye ameshinda kila mkosoaji wa kimadhehebu, ambaye amepata kushinda dhambi zote zinazopendwa za siku hii, za wakati huu tunaoishi sasa, kama alivyofanya katika nyakati zingine zote za kanisa, wale walioshinda katika wakati huo wa kanisa. Wale walioshinda nini? "'Mimi ni tajiri. Sina haja na kitu. Nina... Loo, mimi ni *haya* yote na *haya* yote. Na mimi ni Bibi-arusi. Mimi ni *hiki*. Sina haja na kitu.' Wala hujui ya kwamba wewe ni uchi, kipofu."

173 Mnauona ule wakati wa udanganyifu ambao niliusema? Si kama wale waliokatwa vichwa vyao, huko nyuma, wapate lile jiwe jeupe; si wale waliouawa katika ufia imani, na kuchomwa kwenye nguzo, na vitu kama hivyo; walioshinda taji. Bali ni wakati huu mdanganyifu sasa, unaofikiri ya kwamba wao ni kila kitu. "Vema, mimi ni mfuasi wa kanisa. Mimi ni mtu mzuri. Mimi ni mwanamke mzuri. Ninafanya jambo *hili*. Hainibidi kufanya jambo *Hili*."

174 "Lakini yeye ashindaye," yeye ayashindaye mambo hayo yote ya kilimwengu ya wakati huu, watafanya nini? Wote wataketi pamoja Naye katika kiti Chake cha enzi; wataenda katika Unyakuo wakati Yeye atakapokuja. Loo, jamani! Ninajali nini, basi? Tunajali nini yale ulimwengu usemayo? Tunajali nini yale mtu yeyote asemayo? Roho Mtakatifu mkuu yuko miongoni mwetu. Nguzo Yake ya Moto hututangulia na kutuongoza. Neno Lake linathibitishwa mbele zetu. Upendo Wake umo moyoni mwetu. Ulimwengu uko huko nyuma. Tumepita toka mautini tukaingia Uzimani. Ulimwengu unafikiri wewe una kichaa.

> Lakini inampasa Yesu kuubeba msalaba huu
>   peke yake,
> Na ulimwengu mzima uwe huru?
> Kuna msalaba kwa kila mtu,
> Na kuna msalaba kwa ajili yangu.

175 Miaka thelathini na mitatu hudumani, na msalaba huu uliowekwa wakfu nitaubeba hata mauti itakaponiweka huru.

176 Acha ndugu zangu wanikatae, waseme lolote watakalo, wanikatae kwa lolote. Lakini nitasimama juu ya Neno *hili*, na Hili peke yake.

Msalaba huu uliowekwa wakfu nitaubeba
Hata mauti itakaponiweka huru,
Ndipo niende Nyumbani, katika Unyakuo, nikavalishwe taji.

177 Hilo ndilo sisi sote tunalotaka. Sivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hilo ndilo tunalotaka. Hilo ndilo—hilo ndilo tumaini letu na ombi letu. Hatuna mawazo mengine, ila hilo juu ya Yesu Kristo. Na juu ya haki Yake tunasimama, hiyo pekee, na haki Yake katika Neno Lake. "Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu." Nalo Neno lingali linajithibitisha lenyewe.

178 Kushinda jinsi gani? Kwa kulichukua Neno, ile ahadi, katika unyenyekevu, tukitembea kwa unyenyekevu.

Msalaba huu uliowekwa wakfu nitaubeba
Hata mauti itakaponiweka huru,
Ndipo niende Nyumbani, nikavalishwe taji.

179 Kwa kuwa, "Wakati Parapanda hiyo itakapolia!" Mnaweza kunizika baharini, bali ile Parapanda itaniamsha. Kweli. Ninaenda Nyumbani, siku moja. Amina. Mpaka wakati huo, nitajitahidi, amina, nikiubeba msalaba huu; nikiyaelekeza macho yangu si kwa watu, bali juu ya Kalvari kule ng'ambo, kwa maana Yeye alikuwa ndiye mfano wangu. Alionyesha jinsi ya kufanya jambo hilo. Na mfano Wake, tutaufuata kwa furaha, siku baada ya siku.

Ninamfuata Yesu kila hatua njiani.
Ninamfuata Yesu kila hatua njiani.

180 Hivi hamuupendi huo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Loo, jinsi ninavyofikiri, kumfuata Yeye, siku baada ya siku, kila hatua njiani.

Na tuombe.

181 Bwana Yesu, saa moja na dakika kumi na tano sasa, nikisimama hapa, nikijaribu kulichukua Neno Lako na kuwaelezea watu hawa jinsi ya kushinda. Ulitwambia jinsi ya kufanya jambo hilo. Hukutwambia tu, bali ulituonyesha jinsi ya kulifanya. Ulituongoza. Ulituonyesha jinsi ya kulifanya: kulipokea Neno ndani yetu, na kuhakikisha tunalishika Neno hilo, "Imeandikwa," katika kila jaribio; bali tuwe wanyenyekevu, tutembee kwa unyenyekevu. Ndipo tumeshinda, kupitia Kwako, kupitia nguvu Zako ambazo tayari zimemshinda adui yetu. Na jambo pekee tunalopaswa kufanya ni—ni kutembea tu kwa unyenyekevu na imani, tukiamini jambo Hilo, na beji yetu ya utambulisho wa Roho Mtakatifu, naye Shetani hana budi kuondoka.

182 Kuna leso zilizowekwa hapa. Zinawakilisha wagonjwa. Wana haja, Bwana. Nao wanasoma katika Neno hili lisiloweza kushindwa ambapo walichukua kutoka kwenye mwili wa Mtakatifu Paulo vitambaa na leso. Viliwekwa juu ya wagonjwa.

Pepo wachafu wakawatoka, na miujiza mikuu ilifanyika. Sasa, Wewe ni Bwana Yesu yeye yule leo.

183 Paulo alihubiri Neno hili, na akaandika Neno hili, Neno lile lile tunalojaribu kulifuata. Kwa sababu, alichukua Agano la Kale na kulifananisha, na akaonyesha ya kwamba lilikuwa ni mfano, ya kwamba Agano la Kale lote lililikuwa ni mfano mkamilifu wa hili Jipya. Ee Bwana, jalia tuufuate mfano huo.

184 Tunamwona Bwana wetu, yale aliyofanya. Na tunatambua ya kwamba, hao watakatifu wa Agano la Kale, asubuhi hii, tunaona ya kwamba walienda. Wakati Yesu alipofufuka, waliondoka pamoja Naye. Na, Bwana, tunaamini ya kwamba tutaenda wakati Yeye atakapopiga Parapanda. Tunaamini jambo hilo, ya kwamba Bibi-arusi ataondoka kwenye Siku hiyo na ataungana na—na kundi Lake la Kiebrania, na, pamoja, kutakuwako na Chakula cha Arusi Utukufuni. Hao wanangojea.

Tunaomba sasa rehema Zako na neema juu yetu sisi. Washindi, Bwana, washindi, tunatamani kuwa washindi. Tushinde. Bwana Yesu, Wewe uliushinda ulimwengu. Sasa naomba ya kwamba utamjalia kila mtu hapa, asubuhi ya leo, "Aweke kando kila dhambi, aweke kando kila mzigo utuzingao kwa upesi, tupate kupiga mbio kwa subira katika yale mashindano yaliyowekwa mbele zetu."

185 Paulo alisema haya, Baba yetu wa Mbinguni, pale katika Kitabu cha Waebrania, ya kwamba, "Inatupasa kuweka kando kila mzigo," ule mlango wa 12, ambapo alisema jambo hili, baada ya yeye tayari kuonyesha kwa mfano, kule nyuma: wale walioendelea; wale ambao hawakuendelea; wale waliofuata kwa uvuguvugu; wale waliofuata wakiwa mbele; wale waliosita nyuma. Loo! Yeye alitoa mifano. Ndipo akageuka na kusema, "Na tuweke kando kila mzigo, kila kitu kilicho kidogo sana kituzingacho, tupate kupiga mbio kwa subira katika yale mashindano yaliyowekwa mbele zetu; tukimtazama Yeye, mwenye kuanzisha na mwenye kutimiza Imani yetu, Yeye aliyetupa mfano." Tunafanya hivyo asubuhi ya leo, Baba.

186 Sasa, huku vichwa vyetu vimeinamishwa, sasa chunguzeni kwa makini sana, sana, kwa makini sana. Na, halafu, mwe waaminifu kwelikweli. Inaninii tu—inachuchua tu . . . Hayo tu ndiyo yanayohitajika: uchunguzi wako na uaminifu wako. Kuwa mwangalifu sana unapochunguza sasa. "Nichunguze, Bwana. Nijaribu. Je! kuna uovu wowote ndani yangu? Kama upo, Bwana, jalia niuweke chini, papa hapa sasa. Mahali hapa, ambapo nimeinama, ni madhabahu Yako. Ninauweka chini, papa hapa sasa, ninaweka miguu yangu juu yake. Nitakapoondoka, utakaa pale. Nguvu za Damu Yako zitauteketeza. Ninataka kuwa mshindi. Nina jambo linalonisumbua, Bwana. Ninataka kushinda, asubuhi ya leo. Ninaweza, kwa Wewe. Nimeambiwa hivyo, na Neno Lako. Ninauweka chini sasa, Bwana, na kuweka

miguu yangu juu yake. Ninapotoka kwenye jengo hili asubuhi ya leo, niende, nikijua ya kwamba umewekwa katika pi—pipa la kipausha cha Mungu. Hautakumbukwa tena. Sasa nitautubu na kuomba rehema."

187 Huku vichwa vyetu vimeinamishwa, macho yetu yamefumbwa; mioyo yetu ikiwazia, huo ndio mlango wa kuingilia kwenye nafsi sasa. Je! kuna jambo fulani unalotaka kuweka kando asubuhi ya leo, jambo fulani unalotaka kulishinda? Nawe umelijaribu sana, lakini, asubuhi ya leo, utaacha tu kujaribu. Utakubali tu kile alichofanya. Ninakutaka uinue tu mkono wako, useme, "Bwana, ninataka kushinda. Jambo fulani hunisumbua."

188 Bwana Yesu, unaona mikono hiyo. Sasa, kama mtumishi Wako, anayesimama kati ya walio hai na waliokufa, ninapatiliza kila kitu kinachowasumbua watu hawa pamoja na mimi mwenyewe. Na ninaomba hilo katika Jina la Yesu Kristo, tunaweza kuliacha limewekwa hapa juu ya madhabahu ya Mungu, na kuondoka asubuhi ya leo, huru, kama washindi.

189 Kama dada zetu hawajakuwa na neema huko nyuma, jalia wapewe sasa, Bwana. Kama ndugu zetu hawajakuwa na neema, jalia wapewe sasa. Na ujalie, katika unyenyekevu, mama pamoja na watoto wake, badala ya kuwa wenye majivuno. Yeye anajua ameketi . . . Yeye ni mhubiri kwa watoto hao wadogo. Maisha yake ni mfano. Baba ni mfano kwa mama, kwa kuwa yeye ndiye kichwa cha nyumba. Mama amekuwa akijaribu kumtawala; kamwe hatafanya hivyo tena. Kama mumewe amekuwa akimtumia kama mkeka wa sakafuni, haitafanyika tena. Yeye ni msaidizi. Tujalie, Bwana. Jalia mambo haya yote yanayotuzuia, Bwana, yaondolewe.

190 Tu—tunajiweka wakfu, Baba, kwa ajili ya wakati wa maisha tulio nao mbele zetu, tukijua jambo hili, ya kwamba hatuna budi kufikia mwisho wake, na hiyo ni sasa hivi. Kwa hiyo, asubuhi ya leo, tunachukua nafasi hii, baada ya Ujumbe huu. Tunachukua nafasi hii, Bwana, kuja, kwa sababu tumealikwa kuja. "Mtwikeni fadhaa zenu, kwa maana Yeye hujishughulisha sana kwa mambo yenu." Ninajua Wewe hujishughulisha, Bwana. Ulijishughulisha vya kutosha kufa kwa ajili yetu. Na kweli tunaweza kujali vya kutosha kuja na kukubali yale uliyofia.

191 Tutakase, Bwana. Tujaze upya na Roho Mtakatifu. Jalia Roho Mtakatifu atawale tu mioyoni mwetu, kwa ukuu, tupate kutembea, tukisahau mambo yaliyo nyuma, kinyaa na uchafu tuliyoishi ndani yake wakati mmoja. Tutakaza mwendo tuifikie mede ya wito mkuu, ambako Nuru zetu zinaweza kuangaza katika upendo na unyenyekevu, mpaka kila mpitaji anaweza kusema, "Yule pale Mkristo anayeishi pale kwenye mlima ule. Mtu yule, mwanamke yule, mwanamume yule, ni ua halisi la Mungu lililowekwa wakfu. Hao wana upendo sana na ni

wakarimu sana, daima wamejaa upendo na ni watamu, na wana ufahamu." Tujalie, Baba. Jalia tukolee chumvi, kusudi ulimwengu upate kuona kiu; tujalie, Baba; na tuyashinde mambo ya dunia hii, na masumbuko ya maisha haya. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Ninaweza . . .

Sasa hebu na tuinue tu mkono wetu.

. . . Mwokozi . . .

Akiita kitu gani? "Njoo huku, kutoka kwenye matope." Maisha ya juu zaidi; Kitu fulani kiko ndani yako, kikikuvuta upande huo. Ni kitu gani? Ni Yeye. Huko chini kwenye matope, maua madogo; una Uhai mle ndani, ukijipenyeza kwako. Huo ndio unaokuita, "Panda juu, utoke kwenye matope."

Fuata, fuata . . .

192 Sasa, je! mnamaanisha jambo hilo? Sasa fumbeni macho yenu.

Aniongozako nitafu- . . .

Sasa jisalimishe mwenyewe. Maanisha hilo, sasa.

Aniongozako nitafuata,
Aniongozako nitafuata,
Nitaambatana Naye, Naye, njia nzima.

Aniongozako ni- . . .

Kwa sauti tamu sasa. Kumbuka, jilaze pale.

Aniongoza . . .

"Nitaiweka hapa, Bwana. Nitakufuata Wewe, tangu sasa na kuendelea. Ninalikubali Hilo. Ninaliamini."

Aniongozako . . .

Kumbuka, maisha yako yatashuhudia kwa sauti kubwa zaidi kuliko mdomo wako. Jinsi unavyoishi itathibitisha kwa watu zaidi ya yale unayosema.

Nitaambatana Naye, Naye, (njiani, wapi?) kotekote.

[Ndugu Branham anaanza kuvumisha "*Aniongozako*"—Mh.]

193 Jiweke tu wakfu, kwa kilindi, uaminifu, moyo wako wote. Vipi kama huu ulikuwa ndio wakati wa mwisho ambao ungekubaliwa kuomba? Huenda ukawa. Natumaini sivyo. Huenda ikawa. Basi, uwe na hakika sasa, hakika kabisa, hakika kabisa. Kumbuka, mlango utafungwa, siku moja, ndipo yote yatakuwa yamekwisha. "Omba, utapewa."

[Ndugu Branham anaanza kuvumisha "*Aniongozako*"—Mh.]

194 Wazia tu juu ya utukufu wote ambao alikupa, kila kitu ambacho amefanya. "Ninaamini, Bwana. Ninaamini. Ninaamini ya kwamba Wewe ndiwe mshindi wangu. Ninatembea tu pamoja

na Wewe, Bwana. Ninataka kukaa karibu na Wewe, ili mahali ulipo, ndipo ninapotaka kuwa."

195 Pia kumbuka, Wewe ulitwambia, Baba, ya kwamba, "Tutakuwa pamoja na Bwana milele, tutakaponyakuliwa." Ndiyo kwanza tupate m—mtazamo Wake wa mara moja sasa, wakati akitembea pamoja nasi sasa. Lakini wakati huo tutaninii . . . Ni jambo kubwa jinsi gani, kujua tu ya kwamba Yeye yuko kati ye—yetu! Itakuwaje wakati tutakapokuwa pamoja Naye milele? Tunapenda sana shughuli zetu zote: tunaweza kutoka kwenda kuendesha magari; tunaweza kwenda kununua vitu; tunaweza kwenda kuwinda, kuvua samaki, ama chochote tunachoweza kufanya katika kustarehe. Lakini, loo, kanisa linapofunguliwa, unaona, tunataka kukutana na Bwana wetu. Hilo ndilo jambo kubwa sana kuliko yote. Basi, wazia, Yeye alituahidi. "Na daima tutakuwa pamoja na Bwana. Tutaketi pamoja Naye katika kiti Chake cha enzi, na tuwe pamoja Naye milele." Ee Mungu, kwa unyenyekevu, huku—huku vichwa vyetu vimeinamishwa, tunalikubali, Bwana, katika Jina la Yesu Kristo.

196 Je! unajisikia ya kwamba unaweza tu kuacha, sasa, kila kitu, kila mzigo? Unaweza kutembea tu, juu yake sasa? Kama ndivyo, inua mkono wako, useme, "Kwa neema ya Mungu ninaweka jaribio hili chini. Sitalipiga vita, tena. Nitaushika tu mkono Wake, nianze kutembea."

"Nimepambana, Ndugu Branham. Nimejaribu kuacha kuvuta sigara. Ni—nilijaribu kuacha nywele zangu zikue. Nimejaribu kufanya *hili*. Nimefanya . . . Nimejaribu, kwa nguvu sana, Ndugu Branham. Siwezi kabisa kufanya jambo hilo."

Usilijaribu, tena. Ushike tu mkono Wake, useme, "Baba, Wewe tia mkono wangu katika mkono wa vazi." Unaona? "Nitakupa tu mkono wangu. Nitatembea, Bwana, nikikutegemea Wewe." Itatendeka. Itakuvalisha kama Mkristo halisi. Utakuwa Mkristo halisi.

197 Mpaka nitakapowaona, usiku wa leo, Mungu na awapende na awe pamoja nanyi. Ninyi ni watoto wangu wa Injili. Ninyi ni walionunuliwa.

Sasa ninawarudishia mchungaji wenu, apate kuwaruhusu mwondoke, Ndugu Orman Neville.

NINAWEZAJE KUSHINDA? SWA63-0825M
(How Can I Overcome?)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi, tarehe 25 Agosti, 1963, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2015 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org